# CHUO CHA BIBLIA.

# NYARAKA ZA PAULO KWA WAGALATIA, WAEFESO, WAFILIPI, WAKOLOSAI, WATHESALONIKE WA KWANZA NA WA PILI, TIMOTHEO WA KWANZA NA WA PILI, TITO NA FILEMONI.

# KITABU CHA 14.

# SURA YA KWANZA.
# Waraka Wa Paulo Kwa Wagalatia.

Waraka ambao Paulo aliwaandikia Wagalatia ni tofauti na nyaraka ambazo tayari tumechunguza. Huu ni waraka ambao una uvuvio. Wakati Paulo alipoandika waraka huu, alikuwa mwenye hasira! (Tunaweza kuwa kweli kusema kuwa Paulo alikuwa amejawa na uchungu wa haki alipoandika waraka huu). Ingawa mtumishi huyu wa Mungu alikuwa mara kwa mara akizungumzia shida zilizokumba Kanisa, kwa wakati huu, amefadhaika. Anapowaandikia Wagalatia waraka huu, anazungumzia shida ambazo ni zaidi kuliko dhambi za Wakorintho.

**Injili Kafiri**

Unaposoma waraka huu kwa Wagalatia, unapata wazo la yale yaliyokuwa yametendeka kwa waumini hao. Baada ya Paulo kuhubiri Injili ya 'Wokovu kwa neema kupitia imani, bila cho chote,' viongozi Wayahudi wa Kimasihi katika Kanisa, kama Yakobo, waliyafuata mafunzo hayo ya Paulo kwa Wagalatia, wakifunza wangofu wapya, *'kile Paulo alichowafahamisha ni kweli, lakini hamwezi kuokolewa bila kutahiriwa, bila kufuata amri za Musa.'* Walijaribu kuwafanya Wayahudi kutokana na wanafunzi wa Yesu Kristo.

**Injili Halisi**

Wakati Paulo aliposika kuwa hayo yamefanyika, na kuwa wengi wa Wagalatia ambao walikuwa waumini, hakika walikuwa wanatahiriwa, aliandika waraka wenye masikitiko. Baada ya salamu fupi, anaandika: *'Nastaajabu ya kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe'* **(Wagalatia 1: 6-9).**

Kwa lugha ya Kiyunani, neno la mwisho ni 'laana.' Huu ni ujumbe wenye nguvu sana, ujumbe mkuu kuahi kufanywa na Paulo kupitia nyaraka zake. Paulo anasema, '*kuna Injili moja tu – Injili niliyowahubiria. Watu waliokuwa wakifuata huduma yangu sasa wanahubiri Injili nyingine, Injili ambayo ni kinyume na ile niliyohubiri.'*

Kile anachozungumzia hapa ni ukafiri. Tulikutana na neno hilo katika vitabu vya Sheria na kitabu cha Waamuzi (Kumbukumbu la Torati sura ya kumi na tatu). Ukafiri humaanisha, 'kusimama mbali au kuanguka mbali na kile ambacho awali uliamini.' Paulo aliona ukafiri kama saratani ya kiroho ambayo ni mbaya zaidi kuliko shida za Kanisa la Korintho. Kwa hivyo, anapoandika waraka huu kwa Wagalatia, anakabili injili ya ukafiri ambayo inahubiriwa kwa watu hao kwa kutumia Injili halisi. Waraka huu kisha, unakuwa ujumbe usio wa kawaida wa Injili ya neema Paulo aliyohubiri. Nyaraka zake kwa Wakorintho, Warumi na Wagalatia kwa uwazi zinaelezea Injili aliyohubiri, kisha Yesu akaagiza Kanisa lake litangazie kile kiumbe.

**Mtume Halisi**

Katika sura za mwanzo mbili za waraka huu, Paulo anatoa madai yasiyo ya kawaida kuhusu maisha na huduma yake. Anadai kuwa baada ya kugeuzwa akiwa njiani ya Dameski, aliishi kwa muda wa miaka mitatu akishauriwa na Kristo aliyefufuka, mwenyewe. Pia, anadai kuwa miaka kumi na nne baadaye, alisafiri hadi Yerusalemu na kutiwa mikono na Yakobo, Petro na viongozi wale wengine wa Kanisa kama mtume halisi. Mitume hao waliamua kuwa Paulo angeeneza Injili kwa watu wasiotahiriwa, yaani watu wa mataifa, kisha wale wengine kwa Wayahudi, yaani watu waliotahiriwa **(tazama Wagalatia 2:7).**

Waraka huu wa Paulo kwa Wagalatia ndio tu waraka ambao aliandika kwa mkono wake mwenyewe. Alikuwa na mwandishi wake msaidizi alipondika nyaraka zile nyingine, labda kwa sababu hakuwa akiona vizuri. Sehemu yake ya ‘mwiba ilio kwenye mwili’ ilikuwa uwezo duni wa kutazama kiasi kuwa kipofu (**2 Wakorintho 12:7).** Labda Paulo alikuwa amekasirika alipoandika waraka huu kiasi kuwa hangeweza kugoja msaidizi wake kufika. Alikuwa amepandwa na mori sana alipoandika waraka huu kwa sababu ujumbe wa Neema ambao alikuwa amehubiri kwa Wagalatia ulikuwa umegeuzwa na kukafuriwa.

Kazi: Tanaweza kuona kuwa Paulo alikuwa amekasirika kwa sababu Injili ilikuwa imebadilishwa. Soma waraka huu kwa Wagalatia tena kisha uone kama unaweza kutambua injili ya kwanza yenye ukafiri, kisha injili
halisi ambayo Paulo alikuwa amehuburi. Haya yatakusaidia kuelewa ujumbe wa Paulo na wa Kristo. Linganisha sura hii ya kwanza ya waraka huu na sura ya kwanza ya waraka kwa Wafilipi. Kwa sababu Paulo alikuwa gerezani, ndugu wangofu walikuwa wakihubiri Injili kwa sababu hangeweza kuhubiri mwenyewe. Paulo alishukuru kwa hayo kwa sababu Injili ya kweli ilikuwa inahubiriwa. Linganisha hayo na hisia za Paulo kuhusu Injili iliyokuwa imegeuzwa ambayo ilikuwa inahubiriwa kwa Wagalatia.

## Injili Kwa Kinyume

Katika sura ya kwanza, tunasoma kuwa Injili ya Yesu ndio mwito wa waraka huu mfupi wa Paulo kwa Wagalatia. Kwenye sura ya pili, tunaona maelezo ya kile ninachotaja kama ‘Injili kwa Kinyume.’

Hapa, mafunzo makuu ya Injili ya Paulo yako kinyume sana na yale ya Petro. Hoja hapa ni hali kwamba watu wengi waliokuwa Wayahudi kabla ya kufanyika wanafunzi wa Kristo, walitaka kudumisha asili yao ya Uyahudi hata baada ya kugeuzwa.

Baraza la kwanza kabisa la Kanisa lilikutana huko Yerusalemu mahali swala hilo lilipotatuliwa. Iliafikiwa kwamba, mradi hawaamini tamaduni hizo za Wayahudi kwa wokovu wao, hakukuwa na ubaya wo wote kwa wanafunzi wa Yesu wa asili ya Wayahudi kudumisha mila na desturi zao kama wanafunzi wa Masihi. Lakini pia waliamua kuwa wanafunzi wa Kimataifa wa Yesu hawahitaji kujihuzisha na desturi za Wayahudi. Wanafunzi wa Kiyahudi walifahamishwa wazi wasitwike mzigo huo kwenye mabega ya wangofu wa Kimataifa.

Lakini baada ya baraza hilo la Yerusalemu, hoja bado inabakia kuwa la kutatanisha. Kwa mfano, Kanisa la Antiokia lilikuwa na waumini wengi wa asili ya Wayahudi na watu wa Mataifa. Waliishi kama jamii na walikuwa wakitumia kila kitu kwa pamoja kama chakula. Kwa kuwa mengi ya mambo hayo yaliyotatanisha yalihusu

chakula na ulaji, kadiri ilivyo, walikuwa na meza mbili kila mara wanapotukana kwa chakula. Kwenye meza moja, walikuwa wakitazamia mila na desturi za Wayahudi, ilhali kwenye meza ile nyingine hawakuwa wakifanya hivyo.

Wakati mtume Paulo alipotembelea huko Antiokia, kila mtu alikuwa na shauku juu ya meza ambayo angejiunga nayo. Lakini aliketi kwenye meza ya watu wa mataifa na kula chakula cha watu wasio ya asili yake. Petro alivutiwa na kitendo hicho sana hadi akaamka kwenye meza yake na kuketi pamoja na Paulo kwenye meza ya watu wa mataifa. Kadiri ilivyo, Petro alifanya hivyo kwa muda.

Hata hivyo, siku moja baadhi ya ndugu hao kutoka Yerusalemu, ambao walikuwa wakitazamia amri za Kiyahudi walijitokeza kwenye mlango. Huenda Paulo alikuwa na mgongo wake kwenye mlango, ilhali Petro alikuwa akitazamia upande huo. Wakati alipoona wanafunzi hao wafuasi sugu wa mambo na desturi za Wayahudi kwenye mlango, aliamka kutoka kwenye meza hilo na kuanza kutembea kuelekea meza ya Wayahudi. Baraba, ambaye alikuwa kila mara pamoja na Paulo na Petro kwenye meza hilo la watu wa mataifa, naye alianza kumfuata Petro. Kwa wakati huo, Paulo aligeuza macho yake kwenye mlango.

Paulo alikasirika sana! Anasema kwenye sura ya pili ya kitabu hiki cha Wagalatia, aya ya kumi na moja hivi, *'lakini Kefa alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso wa uso, kwa sababu alistahili hukumu.'* Maelezo asili ya Kiyunani yana dokeza kuwa nyuso zao zilikuwa tu inchi chache wakati wa kushindana huko. Ni kwa hali hii Paulo anatupatia, 'Injili katika kinyume.'

Hapo mwisho wa mashindano hayo pamoja na Kefa yaani Petro, Paulo anatupatia ujumbe mkuu: *'Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure'* ***(Wagalatia 2:20).***

Paulo hakika anasema kuwa, 'Injili inasema kuwa Kristo alikufa ili uweze kuishi. Lakini hapa kuna Injili iliyo kinyume: Sasa ni lazima ufe ili Kristo aiishi.' Tunafahamu kuwa Paulo hazungumzii kuhusu kufa katika sura hii ya pili ya Wagalatia aya ya ishirini kwa sababu kwa mara tatu katika aya hii moja anasema, 'ni hai.' Paulo hakika anazungumzia kuhusu kuishi. Katika aya hii moja, anatupatia sababu tatu kwa nini anaishi.

Kwanza, anasema, *'ni hai kwa sababu ninao katika imani. Mnaishi tele duniani hii ya sasa, nami nitaishi milele kwa sababu ninaishi kwa imani katika Kristo-sio kwa kujaribu kukusukumia hadi mbinguni kwa kutii amri nyingi na sheria.'*

Pili, anadai kuwa, *'naishi kwa sababu Kristo yu hai ndani yangu.'* Paulo atawauliza Wakristo waiozaliwa mara ya pili wa Yesu Kristo hivi, *'Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?'* **(*1Wakorintho 6:19***). Haya ni mafunzo yenye kasi sana*: '… nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu* **(*Wakolosai 1:27).***

Mwishowe, maana ya yale Paulo aliyokuwa akimweleza Petro ni kuwa: *'Ni hai kwa sababu nilisulubiwa pamoja na Kristo.'* Alikuwa akimwambia Petro, waumini wa Antiokia, Wagalatia, na hata mimi na wewe, kuwa tangu Kristo alipokufa ili tupate kuishi; sasa nasi ni lazima 'tufe' ili Naye apate kuishi kupitia sisi. Haya ni sawa na mafunzo ya Paulo katika waraka wake kwa Warumi mahali anaposema, *'Basi, ndugu*

*zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai'* ***(Warumi 12:1).*** Je kweli unaishi kwa sababu unaishi kwa imani? Unaishi kwa sababu ulisubiwa pamoja na Kristo? Unaishi kwa sababu unaamini Kristo alikufa ili uweze kuishi? Unakufa ili Kristo naye aweze kuishi kupitia wewe? Unashuhudia Injili kwa kinyume?

## Injili Kwa Fumbo

Katika waraka huu wa Wagalatia sura ya tatu na ya nne, Paulo anasimulia 'Injili kwa Fumbo.' Kwenye sura ya tatu, anauliza maswali nane. Ikiwa utasilikiza na kujibu maswali hayo ya Paulo, basi utaona kuwa anawasilisha hoja nzito sana ya kufanywa haki kwa imani, wala sio kwa matendo. Paulo anafunza kuwa hatuokolewi kwa sababu tunatii amri za Musa.

Kwenye sura hii ya tatu, Paulo anawasilisha mafumbo mawili. Fumbo la kwanza ni kuwa Ibrahimu, ambaye anatuonyehsa kutokana na ushuhuda wake kuwa imani si hoja kuhusu hekima au matendo; bali ni karama ambayo tunapokea kutoka kwa Mungu. Ibrahimu alipokea karama hii ya imani. Hakupata imani kana kwamba ilikuwa ujira kutoka kwa Mungu. Hii ndio sababu angemwamini Mungu hata alipokuwa mwenye umri wa miaka sabini na tano, naye Mungu akamweleza kuwa atakuwa na uzao ambao idadi yake ingekuwa kama mchanga wa baharini na nyota za mbinguni. Kwa sababu Ibrahimu alimwamini Mungu, naye Mungu alimtangaza kuwa mwenye haki. Katika mfano huu, Paulo anatueleza kuwa tuna imani inayookoa kwa sababu tunaamini Injili ya Kristo, basi sisi nao tu watoto wa Ibrahimu.

Maelezo ya pili ya Paulo anatupatia mtazamo kuhusu kusudi la sheria. Paulo anaandika hivi: '*Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani* ***(Wagalatia 3:24).***' Kwa maelezo mengine, kazi ya torati ni kukuvunja na kukuonyesha kuwa unahitaji Mwokozi. Paulo anaandika: '*…ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure'* ***(Wagalatia 2:21).*** Ukwelu ni, haungeweza kujiokoa kwa sababu haungeweza kutii torati hizo. Torati ilikuwa chombo cha nidhamu kilichotayarishwa kwa wokovu wako kupitia Kristo.

Katika sura ya nne, mtumishi huyu wa Mungu anawasilisha fumbo lingine. Hapa ndipo tunapopata kanuni muhimu sana ya tafsiri ya Biblia. Kuna matukio mengi katika Maandiko ambayo yana historia na fumbo. Fumbo ni hadithi ambayo watu, mahali na vitu vina maana nyingine ambayo yanatushauri kiroho na maadili. Ninaposema kuwa tukio, la mhusika katika Biblia ni fumbo, huwa simaanishi kuwa mtu huyu na tukio hilo sio la kihistoria.

Kwa mfano, Paulo anaandika: *'Ibrahimu alikuwa na wana wawili.'* Hilo ni historia. Lakini, wana hao wawili wanawasilishwa kifumbo. Mwana wa kwanza Ishmaeli (ambaye Ibrahimu alimzaa kupitia mjakazi wake Mmisri, jina lake Hajiri), alikuwa picha ya kazi ya mwili, kumaanisha, *'asili ya binadamu pasipo Mungu.'* Mungu alikuwa akimweleza Ibrahimu kuwa angempatia mwana, naye Ibrahimu alikuwa akijaribu kushikamana na utaratibu huo. Sasa, akiwa na mtoto kutokana na mjakazi wake Hajiri, lingekuwa jambo linalokubalika katika tamaduni za nyakati hizo. Lakini shida lilikuwa kwamba kumzaa Ishmaeli kulikuwa mpango wa Ibrahimu, wala sio wa Mungu. Hadithi ya Hajiri na Ishmaeli ni fumbo la mwili. Unapofanya mambo yako na kuuliza baraka za Mungu juu yake, Paulo anasema kuwa hiyo ni kazi ya mwili.

Tofauti, hadithi ya Ibrahimu kuwa babake Isaka kupitia Sarah ni fumbo la Roho kwa sababu Mungu peke yake ndiye angefanya hayo kutendeka. Tunaambiwa kuwa, *'Basi Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, na umri wao mkubwa, na Sara alikuwa amekoma katika desturi ya wanawake* ***(Mwanzo 18:11).*** Kuzaliwa kwa Isaka kulikuwa mwujiza.

Paulo anawaambia Wagalatia, pamoja nasi kuwa hatuokolewi kwa matendo yetu. Mungu alikuwa atimize wokovu wetu kupitia Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ametupatia karama ya imani na toba ili tuweze kupokea wokovu wa Mungu. Wokovu huo ni karama ya Mungu. Hatujaokolewa kwa sababu tunatii torati ya Musa. Tunatii torati la Musa kwa sababu tumeokolewa. Hayo ndio maana ya Injili halisi katika waraka huu wa Paulo kwa Wagalatia.

Kuwa mwaninifu. Je, umewahi kuwa na wazo kwamba ungekuwa mzuri kiasi kuwa unafuata amri fulani ambazo zimetayarishwa kwa ajili ya wokovu? Kulingana na Paulo, huo ni 'wokovu' ambao ni wa mwili. Injili halisi Paulo aliyohubiri kwa Wagalatia ni kwamba, ni lazima tuzaliwe kimwujiza tena kwa Roho. Huo ni wokovu ambao huko katika Roho.

## Injili Linalovunwa

Paulo anamalizia waraka huu wake kwa Wagalatia wa kutofautisha 'kazi ya mwili' na 'tunda la Roho.' Mwili na Roho ni nguvu mbili ambazo zina fanya kazi-hakika ambazo zinapigana vita-katika maisha ya mwogofu.

Hapa, Paulo anasimulia, 'Injili inayovunwa.' Mfano wa Paulo ni wa kupanda na kuvuna. Ni kama maisha yetu ni bustani. Paulo anasema kuwa katika bustani za maisha yetu, tuna nguvu mbili. Tunaweza kupanda na kutuza kazi ya mwili au tunaweza kupanda na kukuza tunda la Roho. Wakati 'Mbegu' za Roho zinapopandwa kwenye 'bustani' za maisha yetu, matokeo yatakuwa, 'tunda la Roho.'

Paulo anaandika: *'Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria'* ***(Wagalatia 5:19-22).***

Kifungu hiki ni wazi sana kuhusu asili tabia ya wanadamu. Kinatueleza kuwa unapopokea Roho Mtakatifu, asili ya mwili haiondolewi; maovu bado hayo hapo ndani yako. Hapa katika kitabu hiki sura ya tano, Paulo anasema, '*asili hizi mbili zinashindana ndani yako.'* Kuna vita vinavyoendelea katika utu wako wa ndani kila siku.

**Tunda la Roho**

Tunapoingia katika sura ya sita, tunapata maneno haya ambayo yanafahamika sana: *'Msindanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna Maana yeye apandaye kwa mwili atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho, atavuna uzima wa milele.'* Paulo anatueleza kuwa sisi tulio wa Roho tunapaswa kuishi katika Roho, kuenenda katika Roho, kupanda mbegu za mambo ya kiroho katika maisha yetu na kuzalisha tunda la Roho.

**Tazama Ndani**

Kulingana na Paulo, kuna thibitisho tisa za kweli za utukufu kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani yetu. Ikiwa Roho Mtakatifu huishi ndani yetu, tunapotazama ndani, tutagundua tunda za mwanzo tatu za Roho-upendo, furaha na amani.

Upendo ambao Paulo anazungumzia kuhusu hapa ni upendo wa ajabu, yaani upendo wa Agape ambao anaelezea kwenye sura ya kumi na tatu ya waraka wa kwanza kwa Wakorintho. Katika sura hii ya upendo mkuu, anatufahamisha kuwa aina hii ya upendo haivunjiki wala kuharibika kwa sababu haina masharti, na haizuiliki kwa sababu ni uvuvio kwa wale tunaowapenda kwa hali hiyo. Wakati upendo huo unapojitokeza katika maisha yetu, basi huwa hautoki kwetu, bali kwa Mungu.

Paulo anaandika kuwa furaha ni tunda lingine la Roho, ambalo hutokana na ukweli wenye utukufu kuwa Roho Mtakatifu yuko ndani ya mioyo yetu. Paulo pia angeandika wale 'wa furaha' (waraka wake kwa Wafilipi), kutoka gerezani kwa sababu alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Mimi na wewe tunaweza kujazwa na furaha, haijalishi hali inaweza kuwa vipi, kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu. Kwa sababu anaishi ndani yetu, mateso na maumivu hayaepukiki, ingawa mashaka huepukika.

Tunda lile lingine la Roho ni amani. Ikiwa tumepokea Roho Mtakatifu, basi tunaweza kuwa na amani hata wakati haionekani sawa kuwa na amani. Paulo anaita hali hii '*amani ya Mungu ipitayo akili zote'* ***(Wafilipi 4:7).***

**Tazama Kando**

Kwa upendo, furaha na amani ya Roho Mtakatifu, tunatazama ndani. Lakini kwa tunda zile zingine za Roho-uvumilivu, utu wema na fadhili-tunatazama kando. Tutashuhudia tunda hizo za Roho tunapolinganisha na zile zingine.

Ikiwa wewe sio mwenye uvumilivu, na Roho Mtakatifu huishi ndani yako, unakubali kuwa mwujiza ni kiwango cha uvumilivu ambao unatoka kwa Roho Mtakatifu. Unapokuwa na uvumilivu katika ushirika wako na Mungu, uvumilivu huo ni 'imani inayogoja.' Wakati imani yako inapodhihirishwa katika ushirika wako pamoja na watu wale wengine, uvumilivu huo unaweza kutajwa kama 'upendo unaogoja.' Kwa mfano, mara kwa mara inatubidi kugoja Bwana wetu afanye kazi katika maisha ya watoto wetu. Hali hilo inahitaji uvumilivu- aina ya uvumilivu usio wa kawaida ambao ni upendo unaogoja kwa sababu ni tunda la Roho.

Tunda linalofuatia la Roho ni upole. Kuwa mpole humaanisha unawachukulia watu wale wengine kana kwamba wote ni wa jamii yako.

Aina nyingine ya tunda la Roho ambayo inajitokeza katika ushirika ni kiasi. Agano jipya inasema kuhusu Yesu hivi, *'…akazunguka huko na huko akitenda kazi njema…* ***(Matendo ya Mitume 10:38).'*** Kazi njema haituokoi, ingawa sio vibaya kutenda mambo mema au kufanya kazi njema. Msomi mmoja kwa jina *John Wesley* aliwahi kusema, *'Fanya wema wote unao weza, po pote uwezapo, kwa ye yote uwezaye, kila mahali uwezapo, kwa kila njia uwezayo, kwa muda uwezao.'* Fanya tu wema. Kuna kutenda wema, upole na uvumilivu ambao ni tunda la Roho ambayo yanajitokeza tunapotazama kando.

**Tazama Juu**

Tunda za mwisho tatu za Roho- uaminifu, upole na kiasi-hujitokeza unapotazama juu na kutazamia ushirika wetu pamoja na Mungu.

Njia moja ya kuelezea kwa muhtasari maana ya uaminifu ni kwa neno 'tengemeo.' Kabla ya kugeuzwa, wengi wetu huwa hawana nidhamu hata kidogo. Lakini wakati Roho Mtakatifu anapofanya makao ndani ya maisha yetu, tunapata nidhamu na tengemeo katika maisha yetu.

Upole ni tunda lingine la Roho. Upole sio udhaifu. Wakati farasi mwenye nguvu anapotiwa lijamu, huwa hafanywi kuwa dhaifu; bali huwa tu mpole. Wakati Sauli wa Tarso alipokutana na Kristo aliyefufuka akiwa njiani kuelekea Dameski, aya moja ya Biblia lilitafsiri swali Kristo aliyomwuliza hivi: *'kwa nini unapiga mateke miiba?'* Swali hilo lilimaanisha, *'kwa nini unavuta lijamu?'* Wakati Sauli alipojibu, alisema, *'Bwana, nina nini na wewe?'* Sauli 'alivuta lijamu lake' na kuwa mpole.

Wakati farasi mwenye nguvu anapokuwa mpole, huwa anajulikana kama mtulivu. Sawa na mpole, aina hiyo ya utulivu ni nguvu ambazo huwa zimeongozwa. Kuna utulivu ambao ni sawa na upole wakati tunda la Roho zinapoorodheshwa. Ni utulivu ambao ni tunda la Roho katika maisha ambayo yamekubali kuogozwa na Roho Mtakatifu na Kristo aliyefufuka.

Tunda la mwisho la Roho ambalo liliorodheshwa na Paulo ni kiasi. Mkurungezi mkuu wa shirika kubwa, ambaye ana maefu ya wafanyi kazi aliwahi kunukuliwa akisema: *'baadhi ya watu ni kama magurugumu; hawafanyi kazi isipokuwa wasukumwe. Wengine ni kama magari ya kukokota, lazima wavutwe. Ilhali wengine ni kama mwewe, wasipowatia kamba, wanaruka na kwenda zao. Hata hivyo, baadhi yao ni kama saa nzuri sana; dhahabu safi, wako wazi, hutumiza muda, hutengemewa, huwa wanajiuzisha na hufanya kazi vyema.'*

Katika sura ya tano ya waraka huu kwa Wagalatia, mtume Paulo anasema kuwa ikiwa sisi tunamilikiwa, na kuongozwa na Roho Mtakatifu, basi hatutasukumwa, au kukokotwa au kutiwa kamba. Tutafanya kazi kama saa nzuri-kiasi, wanaotengemewa, wanaojiuzisha na kuwa wengi wa kazi njema.

## SURA YA PILI
## Waraka Wa Paulo Kwa Waefeso

Paulo alitumia muda mwingi akiwa mjini Efeso kuliko mahali kwingine alipoanzisha Kanisa akiwa safarini ya Umishionari. Ni hapa Efeso Paulo alipokuwa na 'Seminari' katika chuo cha Tirano ambapo alifunza kuanzia saa tano hadi saa kumi na moja jioni. Huenda wanafunzi wake wa chuo hicho walizidua Makanisa ya mtandao ambayo yaliazishwa huko Efeso, ambayo ndiyo Timotheo aliyoagizwa kuhudumia. Makanisa hayo ya mtandao yalikuwa kwenye miji ya Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Surdi, na Filadelfia, na Laodikia. Makanisa hayo sita halafu Kanisa la Efeso ambayo ndio ya saba, utayapata kwenye sura ya pili na ya tatu ya kitabu cha Ufunuo wa Yohana. Labda waraka huu wa Efeso ulikuwa umeandikwa kwa Makanisa hayo saba pamoja na Kanisa la Kolosai.

Waraka wa Paulo kwa Waefeso unaweza kuwa ndio wa muhimu sana kuwahi kuandika. Kitovu cha ujumbe wa waraka huu wa Paulo kwa Waefeso kinapatikana kwenye sura ya kwanza aya ya tatu: *'Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu*

*Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo.'* Paulo hapa anasema kuwa, '*una baraka zote za kiroho unazohitaji kuishi kama mtu aliyezaliwa mara ya apili, mwogofu anayeozwa na Roho.'* Kisha anatueleza baraka hizo ziko *'katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo'* (aya ya tatu). Paulo anawaambia Waefeso (pamoja nami na wewe) kuwa tunahitaji kila kitu kuishi kama watu wa kiroho hapa duniani. Hata hivyo, baraka hizo za kiroho ziko katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo.

Efeso na Makanisa yale mengine yalikuwa mahali ambapo sasa ni nchi ya Uturuki. Siku za Paulo, sehemu hii ya dunia ilikuwa inajulikana kama *Asia Minor* na ilikuwa mashariki ya milki ya Warumi. Kwa sababu umaribadi wa Efeso ulikuwa sio wa kawaida, na hali kuwa ni pwani ya bahari, wafalme, watu wakuu serikalini na matajiri walikuwa wakitembea huko kwa likizo. Utukufu wote wa Rumi ulifikia kilele wakati Paulo alipofanya ziara huko Efeso.

Kulikuwa na mambo mengi sana ambayo yalikuwa yamefikia kilele huko Efeso wakti Paulo alipofika huko. Leo, mahali kama Efeso, unaweza kuona dhihirsho ya maarifa ya mambo ya kale ya uabudu wa sanamu, uasherati, na picha za ngono. Paulo alikuwa akiwaandikia waumini katika sehemu hiyo ya milki ya Rumi ambao walikuwa wametawaliwa na uasherati kuwa, *'inawezekana kwenu kuishi kama watu watakatifu katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo, katikati mwa milki ya Warumi, mkiwa na uchafu na dhambi hizo zote.'*

Paulo anaandikia kuhusu ushuhuda wa kujipata katika mbingu ya tatu **(*2 Wakorintho 12).*** Wasomi huamini kuwa hayo yalitendeka kwake wakati alipotupiwa mawe huko Listra ***(Matendo ya Mitume 14:19).*** Nafikiri kuwa Paulo kila mara alikuwa akiweka mguu mmoja mbinguni baada ya ushuhuda huo. Anatueleza kuwa hakika, tunaweza kuishi ndani ya Kristo, katika ulimwengu wa roho, ilhali bado tuko hapa duniani. Kwa kuwa Kristo ni wa milele, nasi tu wa milele kwa hali ambayo tunaishi maisha yetu ndani ya Kristo. Paulo anaelezea kuishi huko kama 'ulimwengu wa roho, ndani ya Kristo.'

Sawa na nyaraka zote zake, katika waraka huu, utatambua sehemu ya injili ya utendaji. Waraka huu una sura sita. Baadhi ya wasomi wanaamini kuwa sura za mwanzo tatu ni za injili, au mafunzo ilhali zile zingine tatu, yaani sura ya nne, tano na sita ni za utendaji, au matumizi.

Naamini kuwa sehemu hii ya injili inaendelea kupitia aya ya kumi na sita ya sura ya nne. Katika aya hizo kumi na sita, Paulo anatufunza baadhi ya kweli kuu za Kanisa. Fumbo, humaanisha siri ambalo kitambo kidogo hutambulikana au kufumbuliwa.' Hadi siku ya Pentekoste, hakuna mtu aliyejua kuwa siku moja, Wayahudi na watu wa Mataifa wangekuwa pamoja ndani ya Kristo na kuunganika pamoja katika Kanisa lake. Paulo anatamatisha mafunzo yake kwa kufunza jinsi Kanisa linavyostahili kuhudumu.

Zaidi ya maelezo yenye uvuvio ya Paulo kuhusu asili na kazi ya Kanisa, kuna mwito mwingine katika kitabu hiki cha Waefeso. Kwa kuwa Paulo alitumia muda mwingi huko Efeso-miaka mitatu u nusu- na kuwafunza sana katika 'Seminari,' neno kuu katika aya za mwanzo tatu ni 'kumbuka.' Paulo anawaelezea Waefeso hao waliokuwa na elimu nyingi kuwa tayari wanajua kweli ambazo alikuwa anafafanua kupitia waraka huu.

Baada ya kuwaambia Waefeso wakumbuke yale waliyofundishwa, anaanza sehemu ya utendaji kwenye sura ya nne. Hapa neno kuu ni 'enenda.' Anaandika hivi, '…. *mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitiwa' **(Waefeso 1:4).*** Paulo anawashauri

Waefeso kuenenda kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, wakichukuliana katika upendo na kweli. Kwa maelezo mengine, waenende kwa njia ambayo wanadhihirisha kweli zote alizowafunza alipokuwa huko Efeso.

Unaposoma kitabu hiki cha Waefeso, mwulize Bwana afungue macho yako ya kiroho ili uweze kuishi katika 'ulimwengu wa roho' na 'kwenda kama inavyostahili wito wako ulioitiwa' kila siku.

## Nguo Mbovu Mbovu Na Joho La Heshima

Kusudi la waraka wa Paulo kwa Waefeso ni kuonyesha Kanisa la Yesu Kristo kile lilichotayarishiwa hapa duniani. Waraka huu ni kipeo cha swala la Kanisa. Fanya Waefeso kikutie moyo pamoja na washiriki wale wegnine, kwa neema ya Mungu, Kanisa la halisi ya Yesu Kristo hapa duniani. Hakujawahi kuwa na wakati ambapo dunia nilihitaji shahidi wa Kanisa zaidi kuliko sasa.

Neno halisi, litakupatia mtazamo wa yaliyomo ya kitabu hiki. Neno kuu katika sura ya kwanza ni waza. Paulo anatupatia mambo mengi ya kufikiria hapa kwenye sura hii ya kwanza ya Waefeso. Kwanza kabisa, waza juu ya ysale anayosema kuhusu 'ulimwengu wa roho.' Paulo anatueleza kuwa, katika ulimwengu wa roho, kuna baraka zile za kiroho unazohitaji kuishi maisha yako ndani ya Kristo. Kristo hushi katika ulimwengu wa roho na inawezekana kwetu kuishi naye huko.

Sasa, kila kitu ambacho huishi katika ulimwengu wa roho ni chema. 'Ulimwengu wa roho' humaanisha dunia isiyoonekana ya roho. Katika hali hiyo ya roho, kuna Roho Mtakatifu na mapepo waovu. Tunajulishwa katika waraka huu kuwa mashindano yetu kama waumini ni dhidi ya nguvu za roho katika ulimwengu wa roho. Kulingana na Paulo, muumini ambaye yuko ndani ya Kristo anaweza kushinda nguvu mbovu za giza ambazo huishi kwenye dunia ya mapepo, au katika ulimwengu wa roho.

Waza juu ya yale Paulo anayosema kuhusu utukufu wa Mungu katika sura ya kwanza. Kwenye aya ya kwanza hadi ya sita, kuna baadhi ya jumbe kuu kuhusu Mungu akituchagua kabla ya dunia kuumbwa. Anasema kuwa yalikuwa katika mawazo ya Mungu kabla ya mwanzo kuwa kunafaa kuwa na Kanisa na shahidi wa dunia hii.

Kisha, tambua yale Paulo anayosema katika sura ya kwanza kuhusu utaratibu wa wokovu. Kwenye aya ya kumi na tatu na kumi na nne, tuna picha nzuri sana yake: '*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.'* Haya yote ni njia ya Mungu ya kusema, *'hii ni mali yangu.'*

Pia wazia juu ya sala za Paulo katika Waefeso. Paulo anafanya sala mbili mwafaka sana katika **Waefeso 1:15-23** na **3: 14-21**. Kutokana na sala hizo, ni wazi kuwa alikuwa na orodha ya maombi, na kuwa alikuwa mpatanishi shujaa wa sala. Wakati aliposikia kuwa mtu mmoja amekuja kwa imani na kudhihirisha kuwa hakika walikuwa wanahusika katika kazi ya Yesu Kristo, alianza kuwaombea bila kukoma.

Ni ajabu kulinganisha orodha ya sala zetu na za Paulo. Kiroho, tunawaombea waliopoteza. Paulo alitumia wakati wake akiwaombea watu aliojua kuwa watakuwa washindi wa Yesu. Aliomba kuwa wapokee roho wa ufunuo katika hekima ya Mungu.

Neno lingine kuu ambalo linapatikana kwenye sura hii ya kwanza ni kumbuka. Paulo tayari amewajulisha Waefeso mengi kiasi kwamba kile sasa angewajulisha ni

'kumbuka.' Anawaambia Waefeso hivi, '*kumbuka jinsi ilivyokuwa kabla ya kuja kwa Kristo na jinsi ilivyomaanisha kwako alipokuja katika maisha yako mapya.*'

Katika sura ya tatu, neno kuu ni ufunuo. Kama Farisayo, Paulo alikuwa mtu aliyemchukia Kristo. Hajawahi kuota siku moja kuwa Mungu anawaleta pamoja Wayahudi na watu wasio Wayahudi katika mwili mmoja na kuwafanya kuwa Kanisa la Yesu Kristo. Paulo anawajulisha Waefeso kuwa Kanisa ni ajabu kuu sana ya Mungu.

Katika sura ya nne, Paulo anawasilisha baadhi ya kweli nzuri sana kuhusu tabia ya wanadamu. Naelezea kwa muhtasari sura hiyo kwa neno azimio. Hapa Paulo analinganisha maisha yako ya kiroho na kabati ya kuwekea nguo ndani ya chumba chako. Upande mmoja wa kabati au sanduku hilo, una nguo ambazo ni mbovu mbovu, ilhali upande ule mwingine kuna joho na mavazi mapya ya maisha yako mapya. Matambara ya maisha yako ya zamani ni uongo, hasira, wizi, kuhuzunisha Roho Mtakatifu wa Mungu, uchungu wote, ghadhabu, kelele za matukano, na kila namna ya ubaya **(Waefeso 4: 25-32).**

Mfano huu wa mavazi una tushauri kuazimia kuwa tutavua matambara maovu ya maisha yetu ya zamani. Hatuna haja kuvaa mavazi hayo tena, kulinga na Paulo. Badala yake, anatueleza tuvalie joho za maisha mapya. '*Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli (***24).** '*…mkaseme kweli kila mtu kwa jirani yake* **(**25*). 'Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia'* **( 29).**

**Uwezo Wa Kuwasiliana Na Karama Kuu Ya Kiroho.**

Paulo anasema mawasiliano ni fursa yako ya kujenga yule mwingine na kuleta neema juu yake. Kila mara unapotangamana na mwogofu mwingine, unapaswa kumwacha akiwa amejengeka zaidi kuliko jinsi ulivyompata.

Baada ya Paulo kutueleza jinsi ya kuvalia tena anasema, 'enenda.' Kuishi ndani ya Kirsto ni ushuhuda wa kila siku, 'kuenenda' kwa kila siku. Unaweka mguu mmoja mbele ya yule mwingine hatua baada ya nyingine, siku baada ya nyingine. Hiyo ni hali ya maisha ndani ya Kristo yanavyostahili kuwa.

Mtumishi huyu wa Mungu Paulo anawaeleza Waefeso '*mkaenende katika upendo'* **(*Waefeso 5:2),*** kama vile Kristo naye alivyowapenda. Kisha, *'…enendeni kama watoto wa nuru (8),'* mkihakiki ni nini impendezayo Bwana. Kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli; wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza.

Kisha anasema, *'menende kama watu wenye hekima' (15).* Haya yanamaanisha kutembea ukiwa na kichwa chako wima na macho wazi, ukifahamu haja kuu za dunia hii. Kazi kuu za kijamii, na taasisi kuu za kijamii- hospitali kuu, nyumbani za akina mama wasioolewa, huduma za uokoaji, na hali zote za dunia kwa sababu ya Kristo, na kwa sababu waumini walijua jinsi ilivyomaanisha kuishi katika ulimwengu wa roho, ndani ya Kristo. Ikiwa uko ndani ya Kristo, unakuwa na aina hiyo ya huruma ambayo ni nyepesi, na hamu ya kufanya jambo kuhusu haja za dunia hii. Hii ndio sababu Paulo anasema, *'enenda kama watu wenye hekima.'*

Ni katika hali hii ambapo Paulo anaamuru mfuasi wa Kristo, *'kujazwa na Roho' (18).* Neno la Bwana linasema hivi, '*tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mzajwe Roho.'* Kujazwa na Roho humaanisha kuogozwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anatupatia nguvu za kuishi na kutembea katika ulimwengu wa roho, ndani ya Kristo, licha ya hali yetu.

## Joho La Ushirika

Paulo anatujulisha kuwa Mwenyezi Mungu amewapa *'Watakatifu' kazi ya kutenda'* ***(Waefeso 4:12).*** Hili lilikuwa neno maarufu ya Paulo kwa wale ambao tunaweza kuwaita mashemasi katika Kanisa la leo. Kulingana naye, mwalimu-mchungaji ni 'mkufuzi' lakini wasaidizi wa Kanisa ni wachezaji wa timu. Kusudi la mchungaji linapaswa kuwa kutayarisha, kukamilisha, kutakasa, kuvuvia, kushauri, na kupa changa moto wasaidizi wake kwenda nje na kuhudumu. Hii ni sehemu muhimu sana ya nakala la Agano Jipya ya maana, kazi na kusudi la Kanisa.

Wakati Paulo anapoandika sura ya tano, anatueleza kuwa kazi ya huduma ambayo kupitia kwake watakatifu huanzia mahali palipo pagumu nyumbani. Kwa nini nyumbani ndio mahali palipo pagumu kujumulisha imani? Ni kwa sababu hapo ndipo sisi huwa. Tunaonyesha sehemu moja yetu kwa ulimwengu, lakini mara kwa mara huwa tunaonyesha sehemu ile nyingine nzuri inayovutia kwa jamii zetu. Nyumbani ndio mahali petu, kwa hivyo Kristo anapaswa kwanza kuonekana ndani ya maisha yetu.

Katika **Waefeso 5:21-25,** Paulo anaandika: '*…hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. Enyi, wake watiini wume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.'*

Hapa Paulo anatupa baadhi ya ushauri wa ndoa wa kuvutia unaopatikana katika Maandiko. Anatueleza kuwa wake wanapaswa kunyenyekea waume zao na kuwa watumishi kwao kwa kila jambo. Pia anawaambia waume kuwapenda wake zao '*kama Kristo naye alivyoipenda Kanisa' **(25).***

Wakati Paulo anaposema kuwa, '*mume ndiye kichwa cha mke,* anamaanisha kuwa mume anajukumu kwa mke wake na katika kila jambo katika ndoa na jamii. Hii ndio sababu Mungu anamwambia mke kurahizisha mambo kwa mume wake, kwa sababu ana jukumu kuu. Wakati Paulo anapomwandikia mke, *'kuwa wanyenyekevu kwa mume,'* hakika anasema: Mume wako ameumbwa kuwa vile Kristo alivyo kwa Kanisa, nawe umeumbwa kuwa kwake vile Kanisa ilivyo kwa Kristo. Kwa hivyo, kazi ambayo imetunukiwa mume ni: '**wapendeni (wake zenu), kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa; akajitoa kwa ajili yake; na uwe kwa mke na jamii, kama alivyokuwa.'**

Hilo ni jukumu muhimu sana ambayo imetolewa kwa waume na akina baba, na waume wote wanahitaji kufahamu jukumu hili. Shida kuu katika ndoa ya Wakristo sio wake ambao hawawezi au hawataki kunyenyekea waume zao. Bali, ni waume ambao hawataki kukubali jukumu lao la kutenda, kutoa na kuwa vile Kristo alivyokuwa kwa wake na jamii zao.

Ikiwa wewe ni mume na baba, kubali wajibu wako kuwa yote Mungu anayotaka uwe. Mwulize akupatie nguvu na neema za kuwa vile Kristo alivyokuwa ndani ya nyumba yako.

### Viunganishi Muhimu Katika Ndoa

Wakati Mungu alipoumba ndoa, alifanya ushirika ambao watu wawili watakuwa mmoja katika roho, wazo moja, na umoja halisi. Tunaweza kuwazia hali ambapo waumini katika ndoa watakuwa kitu moja ikiwa tutafikiria kuwahusu wakiwa

wameunganishwa pamoja na pete iliyo na viunganisho tano. Kiunganisho cha kwanza kunawakilisha hali ya kiroho ya ushirika huo- kwamba wanapatikana katika roho moja. Ushurika wa roho ndio msingi wa umoja katika ndoa, na uisiano wa kiroho wa wenzi kwa kila mmoja huwa tu, thabiti ikiwa kila mshiriki yuko pamoja na Yesu Kristo. Umoja wa kiroho unaweza kudhihirishwa kwa mchoro wa pembe tatu, Kristo akiwa juu na mume na mke wakiwa kwenye pembe zile zingine kando. Jinsi wanavyozidi kuja karibu kwa Kristo, ndivyo pia uhusino wao wawili uanvyozidi kusongea karibu na kuwa thabiti.

Kiunganishi kile kingine kinawakilisha mawasiliano, au hali kuwa wao ni kitu moja kwa mawazo. Mawasiliano ni chombo ambacho hudumisha umoja katika ndoa zetu. Ikiwa tuna mawasiliano mema, basi tunakuwa na chombo ambacho tunafanya kazi katika uhusiano wetu wa ndoa. Viini husabaa kwenye giza lakini haviwezi kuishi mahali kuna mwangaza. Mawasiliano huleta nuru katika uhusiano.

Kiunganishi kinachofuatia ni usawa, ambao ni thibitisho la umoja. Mara kwa mara huwa nashangaa kwa nini watu wawili huja pamoja kwa sababu hawana thamani, lengo au hali ya maisha yanayolingana. Wakati msingi wa roho unapokuwa sawa, utapata kuwa usawa unapatikana katika viwango vingi.

Kiunganishi cha kati kati ya viunganishi hivi vitano kinawakilisha upendo. Aina hii ya upendo wa agape, yaani wa ajabu ambao Paulo anaelezea katika waraka wa kwanza kwa Wakorintho sura ya kumi na tatu. Upendo wa agape hauna uchoyo, hauna masharti. Moja ya sababu ndoa humalizika ni watu kuwa wachoyo. Hawajifunzi kuwa na Kristo ndani yao pamoja na watu wale wengine. Wanapaswa kufahamu mafunzo ya Yesu, *'heri kutoa kuliko kupokea.'* Upendo wa agape una kasi ya umoja.

Kiunganishi kingine kinawalikisha ufahamu. Ufahamu ndio nguzo la umoja. Kuna tofauti kati ya wake na waume, na kila mmoja anapaswa kuelewa au kufahamu jinsi yule mwingine anavyojihisi, kufikiria na kutenda. Petro aliwashauri waume kuishi na wake zao, ***'kwa akili'*** **(*1Petro 3:7*).** Kwa maelezo mengine, tambua mume au mke unayeshikiri katika maisha yako naye.

Kiunganishi cha mwisho kinawakilisha umoja halisi wa mume na mke. Ngono ni dhihirisho la furaha la umoja. Ushirika halisi kati ya mume na mke huyo kweli ni aina kuu ya mawasiliano. Ni kupitia ushirika wa ngono mume na mke wanavyodhihirisha yote ambayo yamewakilishwa na viunganishi vile vingine katika pete hii ya umoja.

Wakati ushirika halisi ni vile inavyopaswa kuwa, ngono ni asilimia kumi na uhusiano huo. Basi ikiwa sivyo, inaweza kuwa asilimia tisini ya shida. Mara kwa mara, moja ya sababu kuu kwa nini kuna shida za ngono katika ndoa ni kuwa wenzi hao wanajaribu kudhihirisha furaha ya umoja ambao hauko. Ikiwa hakuna umoja katika roho au mawazo, basi hakuna usawa, upendo au ufahamu wa kuelezea, si ajabu kuwa ushirika kwa ngono una kuwa na ubaridi na upweke?

**Uhusiano Mwingine**

Zaidi ya mkazo huu juu ya ndoa, katika sura za tano na sita, Paulo atazungumzia kuhusu uhusiano wa watumishi na mabwana zao. Kwa kiwango, waumini wanaweza kujumuisha kweli hizo leo kama waajiri na waajiriwa **(tazama Waefeso 6: 5-9).** Watoto na wazazi wao pia wana kanuni za kufuata **(tazama Waefeso 6:1-4).** Katika sura hizi, Paulo anasema kuwa matumizi ya kweli hizi katika waraka huu huanza na mtu aliye karibu sana nawe. Tunaweza kutaja sehemu ya matumizi haya kuwa 'joho la uhusiano.'

Katika sura ya sita, Paulo anatumia maelezo ‘ulimwengu wa roho’ kwa hali ya kinyume. Katika ulimwengu wa mapepo, kuna roho wazuri na wabaya. Paulo anasema kuwa vita ni vya kiroho, na kuwa adui wetu yuko katika ulimwengu wa roho. Adui wetu anasimuliwa kama ni *‘juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho’* ***(12).***

Njia ile tu tunaweza kuishi katika ushindi wa kiroho ni kuwa washindi juu ya nguvu hizo. Kuwa washindi wa kiroho, tunapaswa kutwaa silaha za Mungu **(13-17).** Kila siku ni sharti tutwae silala za Mungu kisha tutoke nje na kupigana vita vya kiroho. Paulo anatueleza kuwa ni lazima tujivunge viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa anjili ya amani, zaidi ya yote tukitwaa ngao ya imani, ambayo ni neno la Mungu; ambayo kwa hiyo, tutaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule muovu. Kila silaha inapaswa kutwaliwa kwa maombi. Silaha hizo tunapaswa kuwa nazo ili kusimame kwa Bwana katika dunia hii yenye dhambi. Tunapaswa kupigana vita, sio kwa nguvu zetu, bali kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Je, unevalia chapeo ya wokovu? Unajua katika mawazo yako kuwa umeokolewa kutokana na nguvu za dhambi? Moyo wako unalindwa na dirii ya haki kifuani? Unatumia ngao ya imani? Unafahamu jinsi ya kutumia upanga wa roho, ambao ni neno la Mungu? Unavalia viatu vya kushiriki katika Injili na wengine? Unavalia silaha ya sala kila wakati katika Roho?

## SURA YA TATU
## Waraka Wa Paulo Kwa Wafilipi

Tunapoanza uchunguzi wetu wa waraka huu wa Paulo kwa Wafilipi, tunapaswa kukumbuka kuwa Kanisa la Filipi liliazishwa kutokana na maono ya mbinguni Paulo aliyopokea. Aliona mtu akisema, *‘Vuka uje Makedonia utusaidie’* ***(Matendo ya Mitume 16:9).*** Kuenea kwa Injili na ustaarabu kutoka Uropa kuelekea upande wa magharibi hadi sehemu hii ya dunia kulitokana na maono hayo ya mbinguni.

Baada ya Paulo kuondoka Filipi, Kanisa la huko Filipi ndio lilikuwa kipenzi chake. Neno lile linaloelezea ushikamano kati ya Paulo na Kanisa la Filipi ni ‘ushirika.’ Paulo anaelezea Kanisa la Filipi kama *‘ushirika wetu katika kueneza Injili’* **(*Filipi 1:5)***. Hili ni picha nzuri sana ya jinsi Kanisa linavyopaswa kuwa. Kanisa kweli ni taasisi ambayo huwa kwa manufaa ya wasio wana chama, kwa sababu kusudi lake ni kutekeleza Agizo Kuu na kuenenza Injili kwa dunia iliyopotea.

Kanisa hilo la Filipi lilikuwa kielelezo cha Paulo kwa sababu lilikuwa la Kimishionari. Unaweza kupata haya katika sura ya kwanza ya kitabu hiki, ikiwa utatambua ni mara gapi Paulo anapotaja Injili.

Waraka huu wa Paulo kwa Wafilipi hakika sio mafunzo; bali ni wa upendo. Ni ujumbe wa shukrani, wa kuvutia na mzuri sana. Kanisa la Filipi ndilo lililokuwa msaada mkuu kwa Paulo, likimsadia kifedha wakati alipokuwa akihudumia watu katika miji nyingine.

Waraka huu wa Paulo kwa wafilipi pia ulikuwa moja ya ‘nyaraka za gerezani.’ Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, Filemoni na Timotheo wa kwanza zinajulikana kama nyaraka za gerezani kwa sababu ziliandikwa wakati Paulo alipokuwa bado gerezani. Waumini wa Filipi walizidi kumsaidia Paulo wakati wa kifungo chake kwa kumtumia vipawa. Basi vile anapowashukuru kwa vipawa hizo, anaandika kuwa *‘havitamani, bali,*

*nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu' (**Wafilipi 4:17).*** Paulo alijua kuwa Mungu anawatuza Wafilipi sana kwa kumtumia karama hizo.

Sura zote nne za Wafilipi zinawakilisha sifa za kuishi maisha ya Kikristo. Mwito wa sura hizo ni 'filosofia na shauku ya kuishi maisha ya Kikristo.' Hapa, Paulo anaonyesha kutokana na maisha yake jinsi ya kuishi kama mfuasi wa Kristo.

Katika sura ya pili, anaandika kuhusu 'mitindo ya kuishi maisha ya Kikristo.' Anatupa mifano nyingi ya watu ambao kweli wanaiga filosofia na shauku ya kuishi maisha ya Kikristo.

Katika sura ya tatu, Paulo anazindua 'kusudi na thawabu ya kuishi maisha ya Kikristo.' Jinsi alivyofanya zaidi ya mara moja kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume, anarejelea tena ushuhuda wake wa njiani kuelekea huko Dameski. Wakati huu anatilia mkazo matokeo ya tukio hilo. Kwa hali hiyo, anatueleza jinsi ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Paulo anataja mwito wa Mungu kama, *'mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Yesu Kristo' **(Wafilipi 3:14).*** Anatueleza jinsi ya kupata thawabu hiyo-jinsi ya kugundua mwito mkuu wa Mungu ndani ya Kristo kwetu wenyewe.

Katika sura ya nne, Paulo anaandika juu ya utendaji, ambayo tunaweza kulitaja kama 'maelezo ya kuishi kama Kristo, kwa hali ya utendaji.' Paulo anatueleza jinsi ya kuishi ndani ya Kristo, na kuweka mawazo yetu juu ya swala ya Mungu katika hali ya amani ya kibinafsi. Kutazamia katikati mwa hali hii, hebu na tutazamie waraka huu wa Paulo kwa Kanisa lake, sura baada ya nyingine.

**Shauku Na Filosofia**

Kwenye aya za ishirini na ishirini na moja za sura ya kwanza, Paulo anaandika: *'Kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini, kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama sikuzote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa mauti yangu. Kwa maana Mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni* faida' ***(1:20-21).***

Kulingana na Paulo, filosofia ya shauku ya kuwa mfuasi wa Kristo inalingana na uangalifu wetu. Kwa hivyo, anaelezea filosofia yake ya kuishi ndani ya Kristo wakati anapotueleza jinsi shauku yake inavyolingana na ukweli kwa uwepo wake gerezani. Mtumishi huyu wa Mungu anaandika: '*nataka Kristo aonekane katika mwili wangu, aidha kwa uzima au mauti, kwa kuwa huru au kufungwa, kwa afya au kuwa mgonjwa. Kama naishi, kudhihirisha Kristo ndio kusudi langu la kuishi. Kwa kufa kwangu, nataka kudhihirisha Kristo katika mauti yangu.'*

Hilo ndio filosofia ya mtu ambaye hakika anaishi maisha ya Kristo.

Zaidi ya kujitolea kwa muumini binafsi, sura ya kwanza ya kitabu hiki inatilia mkazo dhana kuwa maisha ndani ya Kristo ni kama timu ya mchezo. Bwana anataka Kanisa litayarishe watakatifu kwa huduma. Wasaidizi wa Kanisa wanatambua kuwa huduma yote yao imenuiwa kwa washiriki wote wa Kanisa, wakati tutakapotimiza Agizo Kuu na Kanisa la Yesu Kristo liwe hakika kile lilichonuiwa kuwa.

Baadaye, katika sura hilo la kwanza, Paulo anawasilisha maelezo mazuri sana juu ya Kanisa: *'Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkishindania imani ya injili' **(1:27).***

Mtazamo wa Paulo kwa Kanisa aliyonuia unaweza kufafanuliwa kwa kusema: 'Kanisa ambalo kila mshiriki yuko ndani ya Kristo; wote walio katika Kristo wanafanana

kama Kristo; wale walio ndani ya Kristo, ambao ni kama Kristo, huwa kama Kristo kwa pamoja kwa kasi kuwa Injili inaaminika.' Je, Maandiko hayo yanaenda sambamba na sifa za Kanisa ambalo wewe ni mshiriki? Unaweza kusema kuwa kila mshiriki wa Kanisa lako ni mfuasi wa kweli wa Kristo, akiishi maisha ambayo ni ya kiwango moja na Injili? Je, wasioamini wanaamini Injili kwa sababu watazamia jinsi washiriki walivyo kama Kristo katika Kanisa lako wanavyokuwa kama Kristo?

Waraka wa mtume Paulo kwa Kanisa la Filipi unaonyesha kwa mfano, asili, maana na kazi ya Kanisa. Mfano huo unapaswa kuwa kielelezo kwa kila Kanisa, na kwa kila mwanafunzi halisi wa Yesu Kristo, shauku na filosofia ya kuishi kila siku, ndani ya Kristo, kama Kristo.

## Mitindo Ya Kuishi Kama Kristo

Mwito wa waraka huu wa Paulo kwa Wafilipi ni 'kuishi kama Kristo.' Kwenye sura ya pili, Paulo anatupatia mitindo ya jumla ya kuishi kama Kristo. Paualo anawaeleza Wafilipi kuwa kuishi kama Kristo kunahusu kuwa na nia moja nami, nia ya upendo na nia ya unyenyekevu.

Wakati Paulo anapofunza Wafilipi kuwa na nia ya unyenyekevu, anazungumzia juu ya uvumilivu na upendo. Anaelezea juu ya uvumilivu kwa kuandika hivi: ***(Wafilipi 2:3)*** *'..kila mtu amhesabie mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.'* Paulo hazungumzii kuhusu haya na uvumilivu ambao unajenga watu.

Ikiwa una nia ya upendo, basi unazidi haya. Mtu yule ambaye ana nia ya upendo anatumia Amri hii Kuu*: 'Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii'* ***(Mathayo 7:12).*** Paulo anadhihirisha Amri hii Kuu hivi: *'Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine'* ***(Wafilipi 2:4).*** Je, unafikiri juu ya shida zako na mvuto kwanza? Au unatatua shida na mvuto wa watu wale wengine kabla ya zile zako?

Tunapokuwa na nia ya unyenyekevu na wenye upendo, vikwazo vya sifa na uchoyo zinashidwa na tunaweza kuwa na nia moja. Paulo anasema kuwa tunapaswa kudhihirisha kuwa tunaweza kuwa na nia moja na Roho kati yetu **(tazama 1:27).** Wanafunzi wa Kristo mara kwa mara hukabiliana katika Kanisa la Kristo. Mara kwa mara katika makabiliano hayo, utapata, kiburi na tamaa. Kama tutakuwa na nia moja, nia ya upendo na ya unyenyekevu, basi tutatatua shida katika Kanisa zetu.

**Mfano Wa Kristo**

Baada ya kuwasilisha kweli hizo, Paulo anazidi kuelezea juu ya mifano hiyo. Kwanza, kuna mfano wa Kristo **(tazama Wafilipi 2:5-11).**

Yesu hakuwa binadamu. Bali alikuwa mtumishi wa mwanadamu. Alinyenyekea na kuwa mtiifu na mwenye upendo hadi mauti, akifa kwa ajili ya dhambi za dunia. Kwa sababu Yesu alinyenyekea kwa njia hii, Mungu Baba *'alimwadhamisha mno, akamkarimia Jina lile lipitalo kila jina'* ***(9).***

Kulingana na Paulo, sawa na vile Yesu alivyojinyenyekea kwa upendo, pia nasi tunapaswa kuwa hivyo. Hatupaswi kuwa na ubinafsi; bali tunapaswa kuwajali wale wengine na kuwa na nia ya Kristo, kwa upendo ili maisha yetu yawe mfano kwa wale wengine juu ya maana ya kuishi ndani ya Kristo na kuwa kama Kristo.

**Mfano Wa Paulo**

Kwenye sura ya pili, Paulo anawasilisha mfano wake mwenywe. Anaandika hivi, *'nasema, hata nikimiminiwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yetu, na furahi; tena nafurahi pamoja nanyi nyote. Nanyi vivyo hivyo furahini, tena furahini pamoja nami'* ***(Wafilipi 2:17-18).*** Anatueleza kuwa mwenywe, alifuata mfano wa Kristo. Katika kuabudu kwa agano la kale, walikuwa 'wakimiminia dhabihu,' mahali kuhani alipofanyia sadaka hilo. Paulo alijilinganisha na dhabihu hili iliyomiminwa, damu yake ikimiminwa ili Wafilipi waweze kuja kwa imani.

**Mfano Wa Timotheo**

Tena, Paulo anaandika: *'Walakini natumaini katika Bwana na Yesu kumtuma Timotheo afike kwenu karibu, nifarijiwe na mimi, nikijua hali yenu. Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami, atakayeiangalia hali yenu kweli kweli maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo Yesu. Ila mwajua sifa yake, ya kuwa ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili, kama mwana wa baba yake'* ***(19-22).*** Ni wazi kuwa Timotheo alikuwa mtumishi wa Kristo aliyejitolea kabisa.

Hapo mwisho wa sura ya pili, Paulo anawasilisha mfano mwingine wa mzee, Epafrodito, aliyetumwa kumletea matoleo yao gerezani. Tambua jinsi Paulo anavyomwelezea Epafrodito: *'…ndugu yangu, mtenda kazi pamoja nami, askari pamoja nami; tena ni mtume wenu na mhudumu wa mahitaji yangu'* ***(25).*** Kuna viwango vya ushirika ndani ya mwili wa Kristo. Nafikiri kuwa Paulo anatuonyesha jambo kuhusu viwango hivyo anavyosimulia juu ya mzee huyu Epafrodito, kuwa ndugu, mtenda kazi pamoja naye, askari mwenzake, na mtume wao na mhudumu wa mahitaji yake.

Je, viwango hivi vya ushirika vinamaanisha nini? Naamini kuwa, kulingana na nia ya Paulo, ndugu alikuwa mtu mwingine ambaye alikuwa ndani ya Kristo pamoja naye. Kwa Paulo, mtenda kazi pamoja naye alikuwa ndugu aliyefanya kazi pamoja naye, kwa 'kushirikiana' naye, ndani ya Kristo na kwa Kristo. Kwa Paulo, askari mwenzake alikuwa mtu ambaye alihatarisha maisha yake pamoja naye ndani ya Kristo na kwa ajili ya Kristo. Epafrodito bila shaka alikuwa mfano wa viwango hivyo vitatu vya ushirika pamoja na Paulo na kwa kuwa mtume na mhudumu wa mahitaji yake. Ni wazi kuwa mzee huyu ni mfano mwingine mwafaka wa kuishi kama Kristo.

## Thawabu Ya Kuishi Kama Kristo

Tutakapoingia kwenye sura ya tatu ya kitabu hiki, mtume huyu anaandika kuhusu kukumbana na kusudi ambalo Kristo alimkabilia kwenye njia ya Dameski. Katika aya ya tatu hadi ya kumi na moja, Paulo anatueleza kuhusu kubadilishwa kwake kwa hali ya matokeo ya tukio hilo. Anaorodhesha vitu vyote ambavyo kwa wakati mmoja, alionelea kuwa vikuu- wadhfa wake kama Farisayo, kwa mfano. Azimio lake lilikuwa mambo ambayo Paulo alijivunia kabla ya kukutana na Yesu. Lakini wakati alipobadilishwa, mtazamo wake ulibadilika na yote anayahesabu kuwa 'hasara' **(8).** Mungu sasa amempatia mambo ya muhimu sana kufanya. Hiki ni kifungu kikuu sana ambacho mtume Paulo, kupitia mfano wake, anatupatia maelezo mazuri ya kugundua mapenzi ya Mungu ndani ya maisha yetu.

Kwanza kabisa, tambua kuwa Paulo alishuhudia mageuzi yakiwa na azimio, juhudi kuu za kupata kutambua mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Kisha, anatafuta kuwa na kasi ya nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo ndani ya maisha yake.

Ni kama anafanya mbio, na kuna kanuni za mbio hizo. Kushida tuzo hilo, kujua mapenzi ya Mungu, kanuni ni kwamba tunapaswa kuwa watiifu kwa kiwango cha nuru na ufahamivu tulio nao sasa. Ikiwa tutafuata na kutenda katika nuru ambalo Mungu anatuonyesha sasa, basi Mungu naye anazidi kutuoa hadi tuone mapenzi yake kamilivu. Paulo anataja thawabu hilo hapo mwisho wa mbio kama '*mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu'* ***(14).***

Anatupatia baadhi na dokezo kuhusu jinsi ya kutambua mapenzi ya Mungu. Anaandika juu ya kukubadilisha kipao mbele kuwa jambo moja. Jambo hilo ni '*kuyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele'* ***(13).*** Ni ajabu kuwa Paulo angetazamia kipao mbele na kukifanya jambo moja: '*Nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu'* ***(14).***

Je, kuna aina hiyo ya shauku kuu? Una kusadiki kuwa unapokutana na Yesu Kristo, wewe pamoja naye mnakutana kwa kusudi? Unaamini kuwa kuna jambo ambalo anataka umtendee? Unafikia mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu leo, katika Kristo Yesu?

Paulo anatupatia baadhi ya maono jinsi ya kujiuzisha na jambo moja. Sahau mambo ambayo yako nyuma kisha huzidi kuchuchumilia yaliyo mbele. Ishi kulingana na nuru uliyo nayo kisha uzidi mbele katika mapenzi ya Mungu leo, mbele zaidi unavyoweza kuona.

## Maelezo Ya Amani

Paulo anaandika kuhusu amani katika sura ya nne ya waraka huu kwa Wafilipi. Hafikirii kuhusu amani ya dunia, au hata amani na Mungu ambayo Yesu alileta kwetu kupitia dhabihu yake mtini. Bali anashiriki nasi habari njema kuwa kuna ukweli unaojulikana kama amani ya Mungu. Amani ya Mungu ni hali inayozidi amani ambayo Mungu anaweza kutupatia kana kwamba tumetimiza masharti yake. Katika kitabu cha Wafilipi sura ya nne, Paulo anatupatia masharti kumi na mbili ambayo tunapaswa kutimiza ikiwa tutakuwa na kisha kudumisha amani hii.

Sharti yake ya kwanza ni *'msijisumbue kwa neno lo lote'* ***(6).*** Paulo anatueleza kuwa tusijisumbue, kwa sababu kusumbuka sio tu kwa bure, bali pia kuna uharibivu. Masumbuko yanachoma nguvu ambazo unahitaji kukabiliana na shida zako.

Sharti lake la pili kwa amani ni '*Sali kwa kila neno lo lote'* ***(6).*** Haijalishi hali yako ni gani, haijalishi dhiki yako ni nyingi kiasi gani, una fursa ya kumwomba Mungu. Haijalishi matokeo ya sala zako ni kukombolewa kutokana na hali yako ngumu, au neema ya kuishi katika, sala ni muhimu sana. Kwa hivyo, kila mara ombeni kwa neno lo lote.

Shari la tatu la linahusu mawazo. Anasema hivi, *'yatafakarini mambo yo yote yaliyo ya kweli'* ***(8).*** Paulo anatutia moyo kufikiri kuhusu mambo ambayo ni ya kweli, ya heshima, mazuri, safi, ya kupendeza na habari njema. Amua jinsi utakavyofikiri. Mawazo yako ni kama kondoo nawe ndio mchungaji wao. Usiongozwe na mawazo yako.

Hakika, nafikiri kuwa wakati Paulo alipoandika haya, alikuwa akitufahamisha kuhusu msingi ya busara yake. Akiwa gerezani, alihuzishwa kwa kila jambo ambalo lilikuwa si la kweli, yasiyo na heshima, yasiyo haki, wasio safi yenye kuudhi na habari za kuhuzunisha. Ilimbidi kuweka mawazo yako kwenye mambo hayo mazuri ili azidi kuishi.

Jambo la nne ni la utendaji sana. Biblia inasema, *'mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi' **(9).*** Mara kwa mara huwa tunapotoza amani yetu kwa sababu hatuna ujasiri wa kufanya yale tunayojua kuwa ni haki. Maelezo ya Paulo ni kutenda yale tunayojua na kuamini kuwa ni haki **(Saburi 4)**

Tunapata kanuni la tano kwa maneno haya, *'ikiwapo sifa nzuri yo yote,' au 'ukiwapo wema wo wote' **(8).*** Hii ni kumaanisha kuwa tuna hoji thawabu ya mambo mema tuliyo nayo katika safari yetu ya amani. Ilimfaidi nini Paulo kumtumikia Kristo jinsi alivyofanya-katika gereza moja hadi nyingine? Hivi ndivyo Paulo alivyomaanisha kwa kuamini au kutilia shaka wema wetu. Kutilia shaka thawabu ya kazi njema yetu kunaweza kuwa 'mwizi wa amani.'

Kanuni ya sita ni, '*na tushukuru' **(6).*** Amani ya kibinafsi inaweza kuwa matokeo ya mtazamo wetu mwema wa shukrani. Unapodhihirisha kuabudu na shukrani, unakuwa mara moja unachunga mawazo yako mbali na mambo yaliyo kinyume, kuelekea malisho ya majani mabishi. Kuwa na shukrani ni aina ya urekebishaji wa kukusaidia kudumisha hali yako ya ukunjufu.

Hatua ya saba ni radhi. Radhi ni upendo unaosuburi tunapomgoja Bwana. Kutokuwa na radhi ni '*mwizi wa amani.'* Radhi ni tunda la Roho Mtakatifu ambaye huleta amani **(11).**

Kisha Paulo anaandika sharti la nane: *'Upole wenu na ujulikane na watu wote' **(5).*** Huu ni upole wa kukubali. Ukikubali hali katika maisha yako ambazo haziwezi kubadilika, basi amani itafuata. Upole na radhi ni tunda za Roho **(Wagalatia 5:22, 23).**

Katika kanuni zetu za mwisho nne za amani, Paulo anazungumzia uhusiano wetu na Kristo aliye fufuka. Anatupatia sharti la tisa la kuwa: *'Bwana yu karibu' **(5).*** Paulo hakuwa peke yake, ingawa kila mtu aliyefahamu alikuwa amemtoroka alipokuwa aakishi nyakati za mwisho za maisha yake. Nyakati hizo, aliandika kuwa, *'…hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha……..Lakini Bwana alisimama pamoja nami akanitia nguvu….' **(2 Timotheo 4:16, 17).*** Katika hali ngumu, tunaweza kuwa na amani ikiwa tutakumbuka kuwa Bwana anasimama upande wetu na anatutia nguvu.

Kwa hali sawa na hiyo, Paulo anaandika kanuni lake la kumi: *'Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini' **(4).*** Kwa kuwashauri Wafilipi 'kufarihi katika Bwana', Paulo hakika anasema, jifunze kupata furaha yako kutokana na kumjua Kristo.

Pia anaandika sharti lake la kumi na moja kuwa: *'Kama kuna sifa zo zote,'* kumaanisha 'tambua kuthamini idhini au kibali cha Mungu.' Ikiwa utatengemea idhini ya watu wale wengine ili kudumisha ukunjufu wako, basi hali ya ukunjufu huo wako ni dhaifu sana. Kutakuwa na nyakati hautapata kibali cha Mungu na idhini ya binadamu kwa wakati mmoja. Unaweza kuwa na furaha imara na amani ikiwa utajifunza kuthamini kibali cha Mungu. Kuna maneno matatu ambayo yamerekodiwa katika Biblia yanayozungumzwa na Mungu, kwa Ibrahimu. Maneno hayo ni, *'uende mbele yangu' **(Mwanzo 17:1).***

Sharti la mwisho la Paulo kuhusu amani ni, *'Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu'* ***(7).*** Hii ni njia nyingine ya kusema, 'Mungu, siwezi, lakini unaweza. Sio hoja ya mimi ni nini au ni nani; bali wewe ni nini au ni nani. Si hoja kile ninachoweza kufanya; bali kile unachoweza kutenda. Muhimu sio kile ninachohitaji, bali kile unachohitaji. Hatimaye, haitakuwa kile nilichofanya, bali kile ulichofanya.' Hali hii ambayo ninalitaja kama, 'siri nne za kiroho; hutuongoza kwa 'amani ambayo imeshinda ufahamu wetu.' Siri hizi zinadhihirisha maana ya 'kupumzisha roho na nia zetu ndani ya Kristo Yesu.'

Je, una hali inayozidi ya amani ambayo Biblia inataja kama amani ya Mungu? Mwulize Mungu akupatie kipimo cha neema unayohitaji kutimiza masharti hayo. Mungu anaweza kutuweka katika hali moja ya amani ya kibinafsi, lakini hali hiyo ina masharti sana. Tunapotimiza kanuni hizo ambazo Paulo na waandishi wengine wa Maandiko wanazungumzia, Mungu naye anaweza kutuweka katika hali ya amani inayozodi, ya kibinafsi.

## SURA YA NNE
## Waraka Wa Paulo Kwa Wakolosai.

Mji wa Kolosai huko takribani kilomita 160 kutoka mjini Efeso. Inawezekana kuwa Kanisa la Kolosai lilikuwa sehemu ya kundi la Makanisa ya mtandao, ambayo yanatajwa katika kitabu cha (**Ufunuo wa Yohana 2, 3).**

Kanisa la Kolosai ndio lililokuwa na shida chache kati ya Makanisa ya wakati huo. Kwanza kabisa, kulikuwa na shambulizi la kifilosofia, na hekima dhidi ya imani ya Wakolosai. Wayahudi wa Kiorthodox wa Masihi huko Kolosai walikuwa wakijaribu kusukumia amri za Kiyahudi dhidi ya wanafunzi waaminifu wa Kolosai. Mwishowe, kulikuwa na watu katika Kanisa la Kolosai ambao walikuwa wakijiuzisha katika vitendo ambavyo vilihoji kama maono, uabudu wa malaika, na mambo megine yasiyo ya kawaida. Wakati shida hizo zilipojitokeza huko Kanisani Kolosai, Epafras ambaye alikuwa mchungaji katika Kanisa hilo, alimtafuta Paulo huko Rumi ili kupata ushauri wake. Inawezekana kuwa ziara hilo lilisababisha waraka huu wa Paulo huko Kolosai.

Kitabu cha Waefeso kilikuwa mtazamo wa Paulo kuhusu swala la Kanisa. Kitabu cha Kolosai kilikuwa mtazamo wa Paulo juu ya 'Kristo wa Kanisa.' Sehemu ya shambulizi la kifilosofia dhidi ya imani ya Wakolosai lilihuzisha sana mtu wa Yesu Kristo. Watu walikuwa wakimdunisha Yesu Kristo kuliko vile kanuni za imani zinavyothibitisha: 'Mungu yule wa Mungu yule.' Filosofia hii ilikabili hali ya Uungu ya Kristo, hali kuwa Yesu Kristo alikuwa Imanueli, yaani 'Mungu pamoja nasi.' Hii ndio sababu utukufu au ukuu wa Yesu Kristo ndio mwito wa waraka wa Paulo kwa Wakolosai. Katika waraka huu, anasema hivi, 'ikiwa unaye Kristo, basi una kila kitu. Ukikosa Kristo, unakosa kila kitu. Kama Kristo ni cho chote kwako, basi Yesu Kristo ni kila kitu kwako. Kwa sababu, hadi Yesu Kristo awe kila kitu kwako, sio cho chote kwako.'

Katika Kanisa zetu siku hizi, nafikiri kuwa tunaenda sambamba na shida zilizoikuba Kanisa la Kolosai. Tuna watu ambao wanajaribu kuweka mipaka juu ya waumini ambayo ni kinyume na mafunzo kuwa tumeokolewa kwa neema kupitia imani, wala sio kwa matendo. Pia kuna watu Kanisani, ambao hufukiri kuwa kila kitu ambacho ni cha kiroho ni kutoka kwa Roho Mtakatifu, jambo ambalo linawafanya kukosa uthabiti

juu ya sehemu ya giza ya ulimwengu wa roho. Kuna waumini wanaotabiri ambao hushusha imani hadi kuwa kitu ambacho ni kama barafu au ubaridi. Kisha kuna watu katika Makanisa yetu leo ambao wanajaribu kufanya Kristo ndani ya kitu kama unyenyezi, kisichoshikika kama mvuke. Wanafanya Kristo na mafunzo yake kuwa ya kutatanusha kiasi kuwa huwezi kujua yale wanayozungumzia.

Kuna aina ya shida Paulo anazozungumzia wakati anapowaandikia Wakolosai. Katika mafunzo ya Paulo kwenye waraka huu wa Wakolosai, tunafaa kutafuta matumizi ambayo yanaweza kutumiwa kuelezea aina hizo za shida katika Makanisa yetu leo.

Katika sura ya kwanza, Paulo anatupatia baadhi ya jumbe nzuri sana katika agano jipya kuhusu Kristo. Anaandika kuwa, '*Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwepo kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha Kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote' **(Wakolosai 1:15-18).***

Unaona kuwa Paulo anaelezea Kristo kwa njia ambayo anakanusha filosofia hizo juu ya mtu na hali ya Uungu wa Kristo?

Zaidi ya kutueleza Kristo ni nani, tambua kuwa Paulo pia atatueleza vile Kristo alivyofanya. '*Naye alituokaa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuigiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi' **(13-14).*** Je, huyo si ni ujumbe wa ajabu sana kuhusu Injili na kazi ya Yesu Kristo?

Katika sura ya kwanza, Paulo pia anawaeleza Wakolosai jinsi ya kukamilisha yale Kristo aliyotenda wakati anapoandika: *'…mkiudumu tu katika ile imani, hali mmekuwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu…' **(22-23).***

Je, unaelewa Kristo ni nani na yake aliyoutendea? Unaelewa jinsi ya kukamilisha yale Kristo aliyokutendea?

Kisha, tambua kuwa Paulo anakuelezea jinsi ya kuuishi ndani ya Kristo. Anaandika: '*Basi, kama mlivyopokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani' **(2:6-7).*** Huo ni ujumbe mzuri sana kwa hali ya utendaji juu ya jinsi ya kuishi ndani ya Kristo na matokeo ya kuishi yanavyoweza kuwa.

Katika sura ya pili, Paulo atatueleza kile tulicho nacho ndani ya Kristo anapoandika*: 'Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Nanyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka. Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu'* (**9-12).** Paulo anazungumzia maneno haya kwa wana sheria ambao wanawaambia Wakolosai kuwa ni sharti watahiriwe, ili waweze kuokoka.

Waraka wa Paulo kwa Wakolosai unadhihirisha maoni yake ya undani ya kiroho. Moja ya funguo za maisha ya kiroho ya Paulo yalikuwa ni maombi. Anatuonyesha kwa mfano, umuhimu wa sala sawa na jinsi Yesu alivyofanya. Hebu tazama sala ya Paulo kwa waumini katika Kanisa la Kolosai kisha ulinganishe na sala zako. Halafu, jaribu kujifunza

jinsi ya kuomba kama vile Paulo alivyoomba, ukiamini kuwa Mungu anasikia sala zako; na jambo hilo litakusaidia kuelewa na kufuata njia zake.

## SURA YA TANO
## Waraka Wa Kwanza Wa Paulo Kwa Wathesalonike.

Mwito wa waraka wa Paulo wa kwanza kwa Wathesalonike ni kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo. Swala hili lilikuwa muhimu kwa waumini wa Wathesalonike, kwa sababu Paulo aliwaeleza ukweli huu ingawa alikuwa pamoja nao kwa muda mfupi.

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, kuna maelezo mazuri sana jinsi Kanisa lilivyoanzishwa huko Thesalonike **(Matendo ya Mitume 17:1-15).** Aya hizi zinaweza kukusaidia kuelewa huduma isiyo ya kawadia Paulo aliyokuwa nayo katika mji huo wakati Kanisa lilipoanzishwa. Kanisa hili liliazishwa chini ya mwezi mmoja, kwa kuwa Paulo alikuwa huko kwa muda wa majuma matatu. Ingawa alikwenda katika Sinagogi na kuhubiri, wangofu wa kwanza huko Thesalonike hawakuwa Wayahudi, bali walikuwa watu mashuhuri wa asili ya Wayunani. Kutokana na hayo, Wayahudi waliingiwa na chuki sana juu ya Paulo. Walimtesa sana kiasi kuwa aliondoka kwenye mji huo, akielekea huko Berea, kisha Athene na Korintho, mahali alipoandika waraka wake wa kwanza kwa Wathesalonike. Timotheo na Sila walibakia huko Thesalonike na kujiunga naye baadaye.

Lazima Paulo alisisitiza sana juu ya kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo alipokuwa huko kwa majuma hayo matatu. Wakati Timotheo alipojiunga naye huko Korintho, alitoa ripoti kuhusu waumini huko Thesalonike. Alimwambia Paulo kuwa ingawa, wanafunzi wa Thesalonike walikuwa thabiti katika Bwana, Wayahudi walikuwa wakiwatesa kiasi kuwa wengi walipoteza maisha yao.

Pia Timotheo alimwambia Paulo kuwa Wathesalonike walikuwa na maswali mengi kuhusu mafunzo yake juu ya kuja kwa pili. Walikuwa wamehusika sana kuhusu wapendwa wao ambao waliuawa kwa ajili ya imani yao kutokana na dhuluma hizo. Je, wangekosa baraka wakati Yesu Kristo atakaporudi tena kuchukua Kanisa lake?

Kwa mtazamo huo, tambua maneno haya Paulo ambayo yanazungumzia juu ya mjio wa pili wa Yesu Kristo na kunyakuliwa kwa Kanisa. Unyakuzi wa Kanisa ni mafunzo ambayo waumini ‘watapatikana’ huko mbinguni kabla ya Yesu kurudi. Paulo anatuonyesha moyo uliojaa upendo kwa Wethesalonike walioteswa anapoandika: ‘*Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenywe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo.*’

Haya ni moja ya vifungu muhimu sana vya Maandiko kuhusu mjio wa pili wa Yesu Kristo. Tambua uzito wa moyo wa Paulo anapondika kifungu hiki: kama mwalimu

mkuu, Paulo hataki waumini hao wanaoteswa huko Thesalonike kuwa bila ufahamu kuhusu baadhi ya mambo kuhusu mjio wa pili wa Yesu Kristo (**13).**

Kwa kuwa ni mmishionari mkuu, hataki waumini hao wapya wa Thesalonike kuwa bila imani. Kwa maana, anaandika, kuwa ikiwa tutaamini kuwa Yesu alikufa na kufufuka tena, tunaweza kuamini katika ufufuo wa wapendwa wetu waliokufa **(14).** Kisha anawaeleza kwa undani kuhusu kunyakuliwa kwa Kanisa.

Kwa kuwa Paulo ni nabii mkuu, hataki Wathesalonike wawe bila neno kutoka kwa Bwana. Anaandika na kuwaambia, *'kwa neno la Bwana'* (***15).***

Mwishowe, kwa kuwa ni mchngaji mashuhuri, hataki wapendwa hao kuwa bila tumaini au faraja. Labda haya ndiyo yanayotia moyo Paulo kushikiri nasi ukweli huu na Wathesalonike, kwa sababu haja yao ilikuwa wapendwa wao walioliwa. Anaandika hivi, *'Bwana mwenywe atakaposhuka kutoka mbinguni,…waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza' **(16).*** Kunyakuliwa kwa Kanisa ni jambo la funzo la muhimu sana katika kifungu hiki cha Maandiko. Paulo anaandika maana ya mafunzo haya kwa Wakorintho. (**1 Korintho 15:51, 52),** Yesu anafunza kweli huu kwenye mlima wa Mizeituni **(Mathayo 24:40, 41).**

Paulo anafunza matokeo ya kuamini katika mjio wa Kristo tangu mwanzo wa waraka huu kwa Wathesalonike. Katika salamu zake, anaandika: *'Twamshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu nyote, tukiwataja katika maombi yetu. Wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani, na taabu yenu ya upendo, na saburi yenu ya tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo…'*

Paulo alikuwa na sababu ya kutaja 'kazi za imani' na 'taabu ya upendo' anapoandikia Kanisa hili. Kwa sababu Wathesalonike walikosa kuelewa mafunzo yake kuhusu kuja kwa mara ya pili kwa Yesu, kadiri ilivyo, baadhi yao waliacha kazi zao. Walifikiri kuwa mjio wa pili ulikuwa karibu na kuwa waliamua kuishi karibu wakimgoja Bwana aje. Paulo anadokeza, kuwa ikiwa una imani katika mjio wa pili wa Kristo, unapaswa kuhusika katika taabu ya upendo kwa Kristo.

Katika sura ya pili ya waraka huu wa kwanza wa Wathesalonike, tunapata sifa za ajabu sana za Paulo, kielelezo cha Mmisionari. Tambua ujasiri, ukakamavu, uaminifu, uwazi, na unyofu wa Paulo kwa Mungu na kwa Neno la Mungu. Anawaeleza Wathesalonike kuwa kusudi lake la kuishi lilikuwa kunawiri kwao kiroho **(1-12).** Kwenye sura ya tatu, tunapata maelezo ya jinsi waraka huu ulivyofikia kuandikwa, wakati Paulo anaposema: *'Kwa hiyo mimi nami nilipokuwa siwezi kuvumilia tena, nalituma mtu ili nijue imani yenu, asije yule mjaribu akawajaribu, na taabu yetu ikawa haina faida. Lakini Timotheo alipotujia hivi sasa kutoka kwenu, alituletea habari njema za imani yenu na upendo wenu, na ya kwamba mnatukumbuka vema siku zote; mkitamani kutuona sisi vile vile kama sisi kuwaona ninyi. Kwa sababu hiyo, ndugu, tulifarijiwa kwa habari zenu, katika msiba na dhiki yetu yote, kwa imani yenu. Kwa kuwa sasa twaishi, ikiwa ninyi mnasimama imara katika Bwana ' **(5-8).*** Haya ni maono mazuri sana katika moyo mkuu wa Paulo mmishionari, mchungaji, mwalimu, na mwandishi wa nusu ya agano jipya.

Je, unaamini kunyakuliwa kwa Kanisa la Yesu Kristo? Mtume Paulo anashiriki nasi kwa sababu aliataka tufarijiwe. Usikisose faraja ambazo zinaweza kupatikana katika mafunzo ya kunyakuliwa kwa Kanisa. Ni tumaini iliyo na baraka ya wote wanaoamini, na ndio tumaini la dunia hii.

Katika sura ya nne, kuongezea kifungu hiki ambacho tumezungumzia, Paulo anaanza kuwasilisha baadhi ya matumizi ya utendaji ya mafunzo haya. Anaeleza Wathesalonike ambao walikuwa wamestaajabishwa na hali kuwa Yesu Kristo alikuwa arudi tena, kuwa watakuwa mashahidi wema kwa kujitahidi kutulia, na kutenda shughuli zao na kufanya kazi kwa mikono yao wenyewe kama walivyoagizwa **(11-12).**

Katika sura ya tano, Paulo kwanza anazungumzia kuhusu utaratibu wa kuja kwa mara ya pili, kisha anageuka na kuwa mwenye utendaji sana kwa kutilia mkazo wazi na matumizi ya kimsingi kuhusu mafunzo hayo. Anaandika hivi: *'Lakini, ndugu, kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa' **(1-3).***

Katika kifungu hiki, Paulo ni kama anasema kuwa tunapaswa kusadiki kuwa hatuna habari za Mungu wala hatuwezi kuzipata kuhusu hakika ni lini Yesu atakaporudi. Hata hivyo, anaendelea kusema: *'Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi' **(4-6).***

Kando na kunyakuliwa kwa Kanisa, kuna matukio mengine ambayo tunapaswa kutilia maanani kuhusu mjio wa pili, kama ufalme wa miaka elfu moja **(tazama Ufunuo wa Yohana 20:4-6).** Baadhi ya watu huchukulia ufalme huo kwa hali halisi, ilhali wengine huuchukulia kama tarakimu. Ikiwa unasema kuwa ufalme ni wa kiroho au wa tarakimu, basi wewe u wale wanaojulikana kama 'wanaoamini miaka elfu moja.' Ikiwa unaamini kuwa Yesu Kristo yu haja kabla ya kuanza kutawala kwa muda miaka elfu moja hapa duniani, basi nawe uko kikundi cha 'wanao amini kabla ya miaka elfu moja.' Na hatimaye, ikiwa umaamini kuwa mambo haya yatakuwa bora na kwamba ufalme wa Mungu utakuwa wa uhakika hapa duniani, na kwa wakati huo Yesu Kristo atarudi hapa duniani, basi nawe uko kikundi cha, 'baada ya miaka elfu moja.'

Pia kuna wale wanaosema kuwa wao ni 'kila wakati', kwa sababu wanaamini kuwa 'yote' yatakuwa vema. Lakini, haijalishi mtazamo wako wa kithiolojia ni upi juu ya kuja kwa mara ya pili, sehemu ya matumizi ya waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wathesalonike ni ya utendaji, hasa hapo mwisho wa sura ya tano. **(12-22).** Anatoa maelezo ya amri kuhusu tabia ya waumini na matendo yanavyopaswa kuwa katika nuru kuhusu haki kuwa Yesu Kristo anarudi tena.

Kuna kweli mbili ambazo tunapaswa kujifunza na kujumuisha katika maisha yetu kutoka waraka huu wa kwanza wa Paulo kwa Wathesalonike. Kwanza kabisa, Bwana Yesu Kristo yu haja tena; na pili, tunahitaji kutaabika kwa upendo wake tunapomtazamia na kumgoja arudi.

## SURA YA SITA
## Waraka Wa Pili Wa Paulo Kwa Wathesalonike

Waraka huu wa pili wa Paulo kwa wathesalonike ni mfupi sana na uliandikwa punde baada ya waraka wa kwanza. Sura ya kwanza na ya tatu zinalingana sana na sura za waraka wa kwanza wa waraka wa kwanza. Kwa hivyo, kwa kuwa huu ni uchunguzi

wa nyaraka hizi, sitataja kwa undani kuhusu sura hizo. Tunafaa kuzisoma na kujifunza kwa makini, lakini sura kuu katika waraka huu ni ya pili.

Kwenye sura hii ya pili, Paulo anajibu baadhi ya maswali na kuzungumzia utata uliokumba Kanisa lililokuwa bado changa la Wathesalonike. Anaandika hivi: *'Basi, ndugu, tuna kusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo'* ***(1-2).***

Paulo anafanya tofauti hapa kati ya kunyakuliwa kwa Kanisa, ambako aliwaambia juu yake katika waraka wa kwanza sura ya nne, na siku ya Bwana, tukio ambalo limeandikwa kuhusu na manabii kama Yoeli, Sefania na Zekaria. Katika waraka wa pili wa Petro sura ya tatu, Petro pia alibashiri kuhusu tukio hii.

Kunyakuliwa kwa Kanisa na siku ya Bwana sio matukio sawa. 'Siku kuu ya kutisha ya Bwana,' jinsi pia inavyojulikana ni hukumu la mapinduzi makubwa ya mambo ya Mungu dhidi ya ulimwengu. Kunyakuliwa kwa Kanisa ni tukio ambapo Kanisa litaondolewa hapa duniani. '*Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa, kulingana na maneno ya Yesu katika (****Mathayo 24: 40, 41).***

Sasa unaweza kuona kwa nini Wathesalonike walikuwa wamechanganyikiwa. Katika waraka wake wa pili kwa Wathesalonike, Paulo anafanya wazi tofauti kati ya kunyakuliwa kwa Kanisa na siku ya Bwana.

**Kwa Muhtasari**

Hiki ndicho kina cha ukweli mkuu ambao Paulo anashiriki nasi kuhusu tukio ambalo linapaswa kutendeka kabla ya siku ya Bwana kuwadia. Paulo alifunza kuwa siku ya Bwana haiwezi kufika hivi kwa urahisi hadi nguvu za uasi wa sheria ambazo ni kitendo cha Shetani, ambazo sasa zinakabiliwa na nguvu za Kristo, zinakapopewa fursa ya kutawala dunia bila kukwazwa. Wakati haya yatakapotokea, watu watakuwa na hamu ya kufuata mambo ya dhambi. Hali hii inakuwa na kutisha sana. Yule atakayeinukia uongozi na utawala wa dunia kwa wakati huo atakuwa mtu ambaye Biblia inamtaja kama Mpiga Kristo. Mpiga Kristo huyo atajaribu kuchukua pahali pa Kristo wa kweli, akipigana vita naye na wote wanaompenda na kumfuata Yesu Kristo.

Baadhi ya watu huamini kuwa Kanisa litapitia wakati mgumu wa mateso hapa duniani, ilhali wengine hawaamini hivyo. Katika waraka wa kwanza wa Wathesalonike, Paulo anaandika hivi: *'Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala'* ***(5:9-10.*** Kukingana na aya hizi mbili, wengi wa wasomi wa Biblia ambao wanaamini kabla ya miaka elfu moja wanaamini pia kuwa Mungu hataruhusu ghadhabu yake kumiminika juu ya watu wake kama ilivyo katika Mateso haya Makuu. Kupitia unyakuzi, anawakoa watu wake kisha kumiminina ghadhabu yake kwa wasio amini ambao watakuwa wamebakia.

Je, unafarijiwa na maneno hayo? Ikiwa unamjua Yesu Kristo kama mfalme anayekuja wa wafalme na Bwana wa mabwana, ambaye atatawala milele, basi maneno haya ya Paulo ni ya tumaini na faraja. Ikiwa Yesu sio Bwana na Mwokozi wako, basi nao maneno haya ni ya hukumu. Mwamini Yesu kuwa Mwokozi wako. Kariri uaminifu wako kwake kama Bwana wako sasa, na maneno haya yatakuwa baraka yako yenye tumaini- na maneno ya faraja kuu kwako.

# SURA YA SABA.
# Waraka Wa Kwanza Wa Paulo Kwa Timotheo

Waraka wa kwanza na wa pili kwa Timotheo, na waraka kwa Tito zinajulikana kama ‘nyaraka za uchungaji’ kwa sababu ziliandikiwa watu ambao alikuwa ameteua na kufunza kuwa wachungaji. Paulo aliandika waraka kwa kwanza kwa Timotheo na waraka wa Tito wakati mmoja, na nyaraka zote mbili ni sawa. Baadaye, akiwa katika hali mbaya huko gerezani, alipoandika waraka wake wa pili kwa Timotheo, ambao una rekodi maneno yake ya mwisho hapa duniani. Tutachunguza waraka wa kwanza kwa Timotheo kisha waraka wa Tito, halafu waraka mfupi kwa Filemoni na hatimaye waraka wa pili wa Paulo kwa Timotheo.

Timotheo alikuwa amechaguliwa na Paulo kuwa mchungaji wa Kanisa la Efeso. Naye Tito alipekekwa kuongoza Kanisa kwenye kisiwa cha Krete. Tunaposoma nyaraka zilizoandikiwa Timotheo na Tito, sifa mbili tofauti zinajitokeza.

Inakuwa wazi kuwa Timotheo alikuwa kijana, mwenye huruma, na mwepesi ambaye Paulo alimchukua kuwa kielelezo cha mchungaji aliye na upendo na anayejali. Lazima Timotheo alikuwa mtu mwoga kidogo kwa kuwa alihitaji ushauri wa Paulo ili awe mkakamavu na mwenye ujasiri.

Sifa za Tito ambazo zinajitokeza katika waraka huu wa Paulo kwake ni tofauti sana. Tito alikuwa mkubwa na kadiri ilivyo, aliye komaa na thabiti. Tunajua haya kutokana na kazi Paulo alizompatia. Kwa mfano, Paulo alimtumia Tito kuwasilisha ujumbe wa njia ya mkono kwa watu walaokuwa wanateseka sana huko Korintho. Pia alimweka Tito huko kisiwani krete, ambapo palikuwa mahali pagumu sana kuazisha na kuongoza Kanisa. Wakaazi wa huko walikuwa watu katili, waovu na wagumu sana. Tito alikuwa mtu aliyekuwa mzuri sana kwa Paulo kwa kazi hiyo ya uchungaji iliyokumbwa na changa moto.

Kulikuwa na uhusiano wa karibu sana kati ya Paulo na Timotheo, uhusiano wa baba- mwana katika kazi na huduma. Tunawazia kuwa wakati Paulo alipokuwa akifunza kwenye taasisi ya Tirano huko Efeso, Timotheo alikuwa mmoja wa wanafunzi wake. Lakini pia tunafahamishwa kuwa mara ya kwanza Timotheo alikutana na Paulo huko Listra **(tazama Matendo ya Mitume 16:1).** Huenda Timotheo alikuwepo wakati Paulo alipotupiwa mawe katika mji huo na kuachwa maututi. Fikiri, wakati Paulo aliponusurika kimwujiza, mvuto uliotokana na tukio hilo bila shaka ulimwendea kijana huyu Timotheo! Nina dhana kuwa Timotheo kwa ujasiri wake na fadhili, alimtambua Paulo kuwa shujaa wake. Paulo alimteua huko Listra akiwa safarini yake ya tatu ya kimishionari, kwa sababu, tangu wakati huo, Timotheo ametajwa kama sehemu ya timu ya kimishionari ya Paulo.

Wasomi huamini kuwa Paulo aliandika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo baada ya kuachiliwa huru kutoka gereza la Rumi. Nia ya waraka huo ilikuwa Timotheo aweze kujua jinsi Kanisa la Mungu, ambalo ni kinara na msingi wa ukweli, lilivyonuiwa na Mungu kuhudumu. Katika nakala ya Kanisa na waraka wake kwa Tito, Paulo alisisitiza sifa za watu walioogoza Kanisa lazima walikuwa**…(tazama 1Timotheo 3:1-13).**

Watu wengi huamini kuwa Kanisa ni ‘kituo cha kuokoa nafsi.’ Lakini ukweli, Kanisa linakusudiwa kuwa kituo cha kuokoa nafsi ambacho ukweli wa Injili

unatangazwa na watu wa kiroho. Ikiwa Kanisa la kawaida litakuwa kituo cha ukweli, basi linapaswa kuwa na viwango wazi vya kiroho kwa wana chama wake, hasa uongozi wake.

Unapochunguza waraka huu, utapata kweli zingine nyingi zinazotiliwa mkazo. Zinajulikana kama 'misemo ya watakatifu' ya mtume Paulo. Paulo anapowaandikia wachungaji, anawaeleza mara kwa mara, '*huu ni usemi wa imani ulio na thawabu ya ukubaliko wote.'* Kile anachomaanisha ni kuwa, ' *niko karibu kutaja jambo ambalo kweli ni muhimu.'*

Usemi wa kwanza wa Paulo wa imani kwa Timotheo ndio huu: *'Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi' (**1 Timotheo 1:15**).* Kile Paulo anachosema hapa ni kuwa, Bwana alitaka kutoa mfano kwa wenye dhambi. Mara kwa mara watu hufikiria kuwa wenye dhambi wamepita kiwango cha kuokolewa. Kwa watu hao, Paulo anasisitiza kuwa, 'Yesu tayari ameokoa walio na dhambi kubwa hapa duniani. Wakati Yesu aliponiokoa, bila shaka alikuokoa hata nawe!' Kwa sababu alitesa Kanisa, anajichukulia kuwa mkuu wa wenye dhambi.

Katika sura ya pili, Paulo anamweleza Timotheo jinsi Kanisa linavyofanya kazi siku baada ya siku, na kufanya maombi kuwa ndio jukumu la kwanza la Kanisa **(1 Timotheo 2:1).** Wakati Paulo anapoamuru kuwa sala iwe kwa watu wote, anaelezea aina fulani ya maombi. Unaweza kulitaja kama 'sala ya Uinjilisti.' Ni sala kwa watu wote kwa sababu Mungu *'hutaka watu wote waokolewe' **(4).***

Kanisa linapaswa kuwa kinara na kituo ambacho ukweli wa injili unatangazwa (**1 Timotheo 3:15).** Ukweli wa Injili unapaswa kutangazwa kwa sala, kwa sababu ni Roho Mtakatifu tu anayeweza kubadilisha watu na kuwafanya wanafunzi. Kulingana na Paulo, sala katisa Kanisa linapaswa kuwa jukumu la kwanza la mchungaji **(tazama 2:1).**

Waraka wa kwanza kwa Timotheo na Tito zinapaswa kuwa kitabu maalumu cha Kanisa. Paulo alizungumzia maswala mengine yaliyohusu Kanisa. Aliguzia kanuni ambazo hazivurugwi na tamaduni ambazo zinapaswa kujumuishwa kila mahali katika vizazi vyote vya Kanisa. Kwa mfano, kuna kifungu ambacho kinamfanya Paulo kutokuwa maarufu kati ya wanawake. Anaandika hivi: *'Vivyi hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu. Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu' **(1 Timotheo 2:9-12).*** Hivi ndivyo Biblia inavyoelezea.

Paulo hasemi hapa kuwa wanawake hawawezi kuhudumu. Lakini jambo ambalo amelitaja sana katika nyaraka zake ni: 'Kuna amri takatifu ambapo Mume anapaswa kuwa kichwa cha mke. Haya yana maanisha jinsi Kristo naye hutazamia na kuongoza Kanisa lake, mume anapaswa kuchunga na kuongoza mke na jamii yake, pamoja na kuchunga Kanisa lake.

Biblia kwa uwazi inawapa waume jukumu la kuwa kiongozi wa nyumbani na Kanisa. Maandiko yanafunza usawa halisi wa mume na mke mbele za Mungu, lakini haifunzi kuhusu kazi na jukumu za mwanamume na mwanamke. Maandiko yanasema, '*Mungu aliumba mume na mke, na aliumba baadhi ya kazi, jukumu na wajibu wa kila mmoja.'*

Kwa maoni yangu, mwanamke anaweza kufanya huduma ye yote Kanisani mradi awe chini ya uangalizi wa uongozi wa wazee, au kanuni za Kanisa. Kwa hivyo, sioni

sababu kwa nini mwanamke hawezi kuwa mchungaji wa Kanisa, akiwa chini wa uongozi sawa na vile waume wachungaji wanavyokuwa.

Jambo hilo linatufikisha kwenye swala lingine muhimu katika nyaraka hizi. Katika waraka wa kwanza wa Timotheo, utapata maagizo mengi kuhusu viwango vya kiongozi wa Kanisa. Kiongozi ana jukumu la kutawala, kuongoza, au kuchunga kondoo wa Mungu. Aina nyingine ya kiongozi ni mashemasi. Wanaweze kutumikia katika huduma za kiroho au za utendaji, lakini hawana jukumu la kutawala Kanisa. Aina hizo mbili za viongozi wa Kanisa kwanza wanatambulishwa kwetu katika sura ya sita ya kitabu cha Matendo ya Mitume.

Maafisa hawa pia wanatajwa katika vitabu vya kanuni za Kanisa, yaani Timotheo wa kwanza na Tito. Viwango vimefafanuliwa kwa viongozi hawa. Moja ya sababu kwa nini Kanisa halina mazao siku hizi ni kuwa, kitambo sana waliacha kutii viwango vya uwana chama wake, hasa vya uongozi wa Kanisa. Njia muhimu sana Kanisa linavyotangaza Injili kwa kizazi cho chote ni kupitia maisha ya viongozi na washikiri wake. Ikiwa wewe ni kiongozi mzee wa Kanisa, kwa makini na maombi, soma viwango vya kiongozi katika nyaraka hizo za uchungaji za Paulo, kisha umwulize Mungu akupatie neema ya kutimiza viwango hivyo.

Paulo anasisitiza hali kuwa viongozi wanapaswa kuwa watu waliokomaa kiroho na waliofuzu kabisa. Jambo moja ambalo hutatanisha sana ni *'mume wa mke mmoja' **(2).*** Haya yanamaanisha 'mume kuwa na mke mmoja.' Baada ya kusoma maneno hayo kwa lugha asili, sifikirii kuwa yanamaanisha kuwa mwanamume huyu hawezi kuwa na mke mwingine, lakini ni kwamba anaishi na mke mmoja kwa wakati uliopo.

Tambua viwango hivi vya mashemasi sawa na vile vinavyokusudiwa wazee. Pia kuna viwango ambavyo vimetengwa hasa kwa wake na viongozi hao wa kiroho. Huu ni mkazo muhimu katika vitabu vya Timotheo wa kwanza na Tito.

Katika waraka huu, Paulo atamwonya Timotheo kuhusu ukafiri, ambao ni, 'kusimama mbali na yake unayoamini.' Paulo anabashiri kuwa siku za mwisho, kutakuwa na ukafiri mwingi. Ukafiri huja kwa njia mbili-'roho zidanganyazo' na 'imani ya waovu' **(1Timotheo 4:1).**

'Roho zinazodanganya' humaanisha kuwa kila kitu cha kiroho sio cha Roho Mtakatifu. Watu wengi hawakubali tofauti hii. Badala yake, huwa wanajitoa kwa kila roho ambayo inaweza kudanganya watu kutoka kwa imani yao ndani ya Kristo.

Aina ya pili ya ukafiri ambao unazungumziwa na Paulo ni 'imani ya waovu.' Neno la Mungu ni imani ambayo tunapaswa kufunza na kuhubiri katika Kanisa zetu. Pia kuna imani za uongo-'imani za uongo.' Imani hizo hazipatikani katika Maandiko, na hazitoki kwa Mungu. Bali, hutoka kwa Ibilisi, na wengi hudanganywa kwa kanuni hizo. Watu wa Mungu hawapaswi kuhuzisha yale wanayoamini katika wazo kuwa hayako katika Biblia.

Kadiri ilivyo, Timotheo alikuwa na ushuhuda alipotawazwa. Inadokezwa hapa kuwa wakati wazee walipomwekelea mikono Timotheo, kuna kitu kilichopitishwa kwake. Paulo anaandikia kuwa: *'Fanya bidii kwa yale uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee.'* Nafikiri kuwa anazungumzia baashi ya fadhili anaposema, *'ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha' **(13-16).***

Paulo ana baadhi ya mashauri kwa Timotheo kuhusu uhusiano wake na watu katika mwili wa Kristo. Ushauri wa Paulo kwa Timotheo si kana kwamba anamwambia kuwa na uhusino wa 'kitaalamu' bali uhusiano unaojali na wa karibu wa familia.

Paulo anampa Timotheo baadhi ya maelezo kuhusu umuhimu wa kudumisha viwango vya haki ya juu kwa wazee viongozi. Anamweleza kuwa ikiwa kiongozi mzee ametenda dhambi, (bila shaka wao kutenda) anapaswa kukemewa mbele ya wote. Paulo anamwonya Timotheo dhidu ya kuwa na upendeleo kuhusu nidhamu ya Kanisa, hata kama kiongozi aliyechunguzwa ni rafiki yake. Anaandika kuwa: Usimwekee mtu mikono kwa haraka. Utakuwa salama ikiwa utafanya mambo kabla ya kuwekelea mikono juu ya watu ***(1Timotheo 5:17-25).***

Ingawa jambo kuu Paulo analohusika nalo ni kuhusu sifa za watu ambao wataongoza Kanisa, katika sura ya sita, anatoa ushauri mwingine. Kwa mfano, Paulo anampa Timotheo baadhi ya mashauri wa utendaji kuhusu watumishi. Anamwambia awaamuru watumishi kuwa wanapaswa kutii mabwana wao ili jina la Mungu lisitukanwe **(1).** Paulo alifahamu kuwa baadhi ya shida za kijamii hazikuwa zimalizike kabisa. Wengi wa waumini wa zamani walikuwa watumishi, na kwa kuwa bado hawakuwa huru hapa duniani, anawaonyesha jinsi ya kukabiliana na utumwa wao.

Katika sura hii, pia tunapata kifungu kizuri sana kuhusu utauwa na kuridhika. Kuna mkazo katika tamaduni zetu ambao unasisitiza sana kuhusu utauwa. Mtoto anapokuwa mchanga akihudhuria shule, anafunzwa kuweka thamani yake juu ya utauwa. Lakini akiisha kuwa mzima, hili linathibitika kuwa sio njia kamili ya kuridhika. Kuna watu wengi ambao huwa wazuri sana katika taaluma zao lakini hawama imani, timizo au furaha katika yale waliyoafikia. Nafikiri kuwa watu kama hao wako tayari kusikia neno la Paulo: ‘*Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa’* ***(6).***

Paulo kisha anaendelea kushiriki nasi baadhi ya onyo kuhusu mali anaposema: ‘*Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatowazo wanadamu katika upotevu na uharibifu maana shina moja ya mabaya ya kila namna ni kupenda fedha…’*

Paulo anamshauri Timotheo *‘kuyakimbia mambo hayo; ukafuate haki…’* ***(11).***

Kisha anazibi kumshauri kwa yale ambayo yatawakumba matajiri: *‘Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atoaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha’* ***(17).***

Maandiko hayasemi kuwa ni vibaya kuwa tajiri. Wengi wa watu wamcha Mungu katika Biblia walikuwa matajiri sana, akiwepo Ibrahimu, Ayubu na mfalme Daudi. Muhimu ni nia ya kutafuta utajiri huo, kisha mtazamo kuhusu mali. Wale ambao ni matajiri wanapaswa kutumia mali yao kwa matendo mema, wakitoa kwa furaha kwa wale walio na haja. Paulo anataja aina hiyo ya kutoa kama kuweka akiba ya milele (**18-19).**

Changa moto ya Paulo kwa Timotheo pamoja nasi kwa jumla ni ‘kujizoeza kupata utauwa,’ kwa sababu utauwa utatufaidi katika maisha haya na yanayokuja **(1 Timotheo 4:8).** Je, unapata mazoezi yanayofaa kujenga utauwa wako katika maisha? Tamadumi zetu zinatufahamisha kujizoeza katika utauwa. Paulo anatushauri kutafuta kuridhika. Je, unatafua utauwa, au unatafuta kuridhika?

## SURA YA NANE
## Waraka Wa Paulo Kwa Tito

Mkazo wa waraka wa Paulo kwa Tito ni kuwa maono ya Kiungu humaanisha wasimamizi wa Kiungu. Ni kama Paulo alikuwa akisema, ‘njia ile ambayo unaweza

kuazisha Kanisa huko Krete, Tito, ni kuwa msimamisi wa Kiungu ambaye atafuta kanuni za Mungu kwa maisha yao matakatifu.' Dhana hapa ni kuwa, 'pamba kanuni za kuridhika' ndio mwito wa yale Paulo aliyomwandikia Tito katika nakala hii ya mchungaji kwa kuazisha Kanisa mahali palipokuwa na ugumu.

Paulo anamweleza Tito kuwa, '*kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru' **(1:5).*** Mtatuzi wa shida za Paulo, Tito aliamrushwa kutatua shida katika Kanisa la Krete ambazo zilikuwa sawa na zile zilizokumba Kanisa la Wagalatia. Wayahudi wafuasi wa imani ya Kiorthodox wa Masihi walikuwa wakiwafunza watu wa huko Krete ili waweze kupata fedha kutoka kwao. Wale wengine walikuwa wakifunza waumini hao wa Krete wapishwe tohara ili waweze kuwa wanafunzi halisi wa Yesu. Hizi ndizo zilizokuwa shida mbili ambazo Pualo alitaka kuzungumzia kwa Tito.

Kifungu kilicho muhimu katika waraka huu wa uchungaji kinasimulia hali tatu za Mungu, kupitia Kristo, hapa duniani. Chunguza ikiwa unaweza kupata jumbe hizo ndio nzuri sana katika Injili ya Agano jipya.

*'Maana neema ya Mungu iwaokowayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwegu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ua utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenywe, wale walio na juhudi katika matendo mema. Nena maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote; asikudharau mtu awaye yote' **(2:11-15).***

## Kanisa La Kuonekana Mara Tatu Kwa Mungu

Je, umewahi kusikia kuhusu Kanisa ambalo limepewa jina, 'Kanisa la kuonekana mara tatu kwa Mungu? Neno 'kuonekana' limetokana na lugha ya Kiyunani. Kuna hali ambapo Kanisa lililozungumziwa na Paulo katika waraka wake kwa Tito linaweza kutajwa kama 'Kanisa la kuonekana mara mbili kwa Mungu,' kwa sababu Paulo anamwandikia Tito kuhusu kuonekana mara mbili kwa Mungu. Anaandika kuwa Kanisa lilinuiwa kudumu katika hali mbili. Paulo anaandika hivi, *'maana neema ya Mungu iwatokayo wanadamu wote imefunuliwa' **(12).***

Neema hii ilifunuliwa wakati Yesu Kristo alipozaliwa huko Bethlehemu na litafunuliwa tena wakati atakaporudi. Kanisa linadumu katika hali mbili za Mungu kupitia Kristo. Katika waraka huu, Mungu anamfunulia Paulo jinsi anavyotaka Kanisa lake liwe kati ya mafunulio hayo mawili. Kwa wakati huu, tunapaswa kuishi, *'kwa kiasi, na haki, na utauwa' **(Tito 2: 12).***

Paulo anatujulisha kuwa katika kufunuliwa kwa kwanza kwa Kristo, ambako kulileta wokovu, Mungu aliwaokoa watu wake kwa sababu alitaka kujisafishia watu hao wawe milki yake mwenywe, wale walio na juhudi katika matendo hayo **(14).** Tuko hapa kuwa watu maalumu ambao wanafarijiwa kwa mfano wa Kristo.

Sasa unaweza kuona kwa nini nilisema kuwa kichwa mwafaka kwa waraka huu wa Paulo kwa Tito kinafaa kuwa, 'Kanisa la kufunuliwa mara tatu kwa Mungu.' Kati ya kufunuliwa kwa kwanza na mjio wa pili wa Kristo, kuna kuonekna kwa tatu-kuonekana kwa Mungu hapa duniani kupitia mimi na wewe. Mungu ametuchagua mimi na wewe kutenda kazi yake. Tuko hapa kuwa watu wake maalumu.' Tunapaswa kuwa na Yesu wa

ndani yetu. Tunapaswa kuwa vyombo ambavyo kupitia kwa Kristo aliyefufuka anajitokeza hapa duniani.

Mkazo wa Paulo katika waraka wake kwa Tito ni kuwa, watu maalumu ambao wanafanya Kanisa la Kristo, wanapaswa, '*kupamba imani ya Kristo'* wakiwa na uzima mtakatifu, wa Uungu, kuwa Mungu anaweza kujitokeza hapa duniani kupitia Yesu Kristo ndani yangu na yako. Tunaweza kuhakikishiwa kuwa Mungu yuko na mipango mikuu kwa maisha yetu, kwa sababu ametuchagua kuwa sehemu ya watu wake maalumu, walio na uzao ambao kupitia kwao, anaonekana hapa duniani.

## SURA YA TISA
## Waraka Wa Paulo Kwa Filemoni

Filemoni ndiye kwa nne katika nyaraka tano Paulo alizoandika akiwa gerezani. Ingawa waraka huu ndio mfupi sana wa Paulo, ni mrefu kwa hali ya utendaji, hasa katika eneno la matendo ya kijamii.

Filemoni alikuwa tajiri asiyekuwa Myahudi ambaye alikuwa muumini ambaye aliishi huko Kolose. Alimiliki watumishi, akiwa na mmoja kwa jina Onesimo. Jina Onesimo lilimaanisha 'kufaa' au 'mwenye faida.' Alipewa jina hili kwa sababu alikuwa mtumishi mwenye faida sana.

Kadiri ilivyo, Onesimo aliiba fedha kutoka kwa bwana wake Filemoni na kutorokea mbali. Kisha, akawa mtumishi mkimbizi na mwizi. Lakini akiwa mjini Rumi, Onesimo alikutana na Paulo gerezani, kisha Paulo akamwongoza katika imani ndani ya Kristo. Kuzaliwa mara pili kunahusu kutoa, na kwa Onesimo, toba ilimaanisha kurudi kwa bwana wake na kukabiliana na malipo yake kama mtumishi aliyekimbia. Lazima Paulo ndiye aliyemweleza hayo. Lakini, pia alimwambia Onesimo kuwa atamtuma kwa Filemoni waraka ukimsihi kuwa mpole kwa ndugu yake mpya ndani ya Kristo.

Waraka huu wa Paulo kwa Filemoni ndio ule Onesimo aliompelekea bwana wake kwa mkono wake alipokuwa akirudi huko. Sio tu waraka ulio na matumzi mengi ya kijamii, bali pia ni kipeo kikuu cha ubalozi na hekima. Unapotambua kuwa kusudi la Paulo kuandika waraka huu, pia tambua jinsi kwa hekima na utaarabu mwingi anapoishughulika swala hili. Anasihi roho ya Filemoni ambayo ni kama ya Kristo, na kutilia mkazo yaliyo mema anapotumahi kuwa Filemoni anamkubalia tena Onesimo kwa moyo mkunjuvu.

Kina cha waraka ni kuwa Paulo anasema kwa Filemoni, na hata sisi kwa utendaji kuwa, Yesu Kristo hubadilisha watu. Anapofanya hivyo, Paulo anamwandikia Filemoni kuwa, '*ningetaka umsamehe Onesimo na kukubali tena, sio kama mtumishi aliyetoroka na mwizi ambaye anapaswa kuadhibiwa, bali kama ndugu, mwanafunzi mwenzako wa Kristo.'* Hukumu iliyokubalika kwa mtumishi aliyetoroka ilikuwa ni kifo.

Je, Yesu amekubadilisha? Yesu amebadilisha uhusiano wako wote? Una imani ya kuamini kuwa anaweza na kuwa atatenda hivyo? Yesu Kristo ndiye tu anawezaye kubadilisha sisi, na uhusiano wetu kwa sababu ndiye tu anayebadilisha watu.

Tunaposoma waraka huu, kuna matumizi mengine ambayo tunaweza kuzoa. Watu wengi huamini kuwa waraka huu wa Paulo kwa Filemoni ulikuwa umejaa ishara. Kwa mfano, wanaamini kurudi na kusamehewa kwa Onesimo kifumbo humaanisha kukombolewa kwetu. Kukomboa kitu humaanisha kukinunua tena na kukihifadhi. Damu ya Yesu Kristo iliyomwangika mtini ilikuwa thamani ambayo alilipa ili Mungu aweze

kutununua na kuturudisha tena kwake mwenyewe na kiwango cha uzima anachonuia tuishi.

Pia kuna picha katika waraka huu mfupi ya jambo ambalo hufanyika kwa watoto wetu. Paulo anamwandikia Filemoni kuwa labda amekuwa ametengwa na Onesimo kwa muda, ili awe naye milele **(15).** Mara kwa mara sisi kama wazazi, tunatengwa nao kwa muda. Kama *'tukiwalea katika njia iwapasayo,'* ***(Mithali 22:6),*** wanaweza kukosa kabla ya kuamua jinsi watakavyoenda katika maisha yao. Lakini wanapoturudia, baada ya kupata imani na ujuzi, wanaweza kujisimamia na kuendelea na maisha yao.

Baadhi ya wengine pia wanaamini kuwa waraka huu unaelezea 'malipo ya kubadilisha.' Wakati mtume Paulo anapomwambia Filemoni, '*na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu'* ***(Filemoni 1:18),*** tuna wale ambao huamini kuwa hiyo ni picha ya yale Yesu Kristo aliyotutendea. Wakati alipokufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, alisema kwa Baba yake kuwa, *'cho chote wanachokwia, ukiandike juu yangu. Mwenyewe, mimi nitalipa.'*

Unaweza kuona kuwa waraka wa Paulo kwa Filemoni umejaa matumizi.

Kuna wazo moja zaidi ambayo tunapaswa kutilia maanani katika waraka huu mfupi wa Paulo kwa Filemoni. Ni wakati Paulo anapomwandikia kuwa, *'nakuwia hata nafsi yako'* ***(19).*** Kulingana na yale Paulo aliyomwandikia Filemoni, hatuwezi kuwa wenyewe hadi tunapozaliwa mara ya pili. Ni kwa sababu Filemoni alikuwa amezaliwa mara ya pili Paulo akasema, '*nakuwia hata nafsi yako, Filemoni. Haungekuwa jinsi ulivyo bila kuzaliwa upya. Kwa kuwa nilikuwa mtendi wa* kuzaliwa kwako kupya, nakuwia nafsi yako.'

Watu wengi wamedhulumiwa na kudunishwa na kukoseshwa furaha kwa sababu wenyewe sio wale Mungu alikusudia wawe. Waraka huu unatufahamisha kuwa hatutawahi kuwa yule, kile, na pale Mungu aliponuia tuwe hadi kutatakuja kwa imani katika Yesu Kristo.

## SURA YA KUMI
## Waraka Wa Pili Wa Paulo Kwa Timotheo

Waraka wa pili wa Paulo kwa Timotheo ndio wosia wa mwisho na agano lake. Historia ya Kanisa inatufahamisha kuwa, baada ya kuachiliwa kutoka gerezani huko Rumi, Paulo alifanya kazi ya umishionari nchini *Spain*, kisha akarudi Efeso. Kutoka Efeso, alienda Troas, akawa huko wakati mfalme wa milki ya Rumi, Nero alipochoma mji wa Rumi na kuwalaumu wanafunzi wa Yesu Kristo. Wakati tukio hilo lilipotendeka, wafuasi wote wa Kristo katika milki hiyo walitangazwa kuwa waasi, na kutendewa ukatili wa hali ya juu sio tu na serikali ya Rumi, bali pia na wana nchi ya mji huo. Kwa kuwa Petro na Paulo walikuwa maadui walioorodheshwa nabari moja na mbili, punde Paulo alitiwa baroni tena.

Ni wazi kutokana na jinsi Paulo alivyotiwa baroni, kuwa hangestahimili kifungo hiki **(2Timotheo 1:4).** Paulo anapoandika waraka huu kwa Timotheo, anafahamu kuwa atauawa. Jambo hili linafanya maneno yake ya mwisho kuwa ya kusikitisha sana.

Kama ungetembelea gereza la *Mamertine* mjini Rumi sasa, ungekubaliana nami kuhusu uzito wa maneno hayo ya mtume Paulo. Jinsi alivyofungwa kwa pete iliogezea mateso yake. Ngome hilo lilikuwa mahali penye uvundo na pa kusikitisha sana. Palikuwa pametengwa kwa wafungwa waliochukiwa sana katika mji huo.

Kwa hali hii, ni ajabu jinsi Paulo alivyoweza kuandika waraka huu wa pili kwa Timotheo na kuweza kupitisha hadi nje ya gereza hilo. Kila mtu, inaonekana kuwa, walikuwa wamemtoroka Paulo, ila mzee mmoja kwa jina Onesiforo na daktari wake mpendwa Luka. Inawezekana kuwa aidha Luka au Onesiforo alipitisha waraka huo hadi nje. Ni wazi pia kuwa Paulo hangeweza kuandika kwa mkono wake, bali alifanya imla.

Unaposoma maneno haya ya mwisho ya Paulo, isisahau hali ya gereza hili ambayo ndani yake, Maandiko haya yaliweza kuandikwa kutoka ndani ya moyo wake:

*'Kwa sababu hiyo nakukumbusha uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu. Maana Mungu hatakupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi' (**2 Timotheo 1:6-7).***

Unaweza kusema kuwa sifa za Timotheo zinajitokeza katika aya hizi. Bila shaka Timotheo alikuwa ana ona haya, jambo ambalo lilimfanya kukumbwa na shida ya kushirikiana na watu. Paulo anadokeza kuwa mwujiza umetendeka katika mikono yake ambaye aliwekelea juu ya Timotheo wakati wa kutawazwa kwake. Paulo anaandika hivi, *'basi usionee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu.'*

Katika sura ya pili, tutaona baadhi ya maelezo ambayo yanaleta mwangaza juu ya maana ya kuwa na uhusiano wa kweli na Kristo. Kwenye aya ya nne hadi ya saba, Paulo anatoa baadhi ya maelezo ya askari, mwana michezo na mkulima.

Matumizi ya wazi ambayo Paulo anafanya hapa kuhusu askari ni kuwa: Wakati mtu anapoenda vitani, hajitii katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika. Bali huwa anajitolea kabisa kwa mambo ya vita. Paulo anamtia moyo Timotheo kujitolea kabisa kwa vita vya Yesu Kristo.

Kisha, anatoa maelezo mengine ya mwana michezo, kwa kusema, '*hata mtu akishindana katika machezo hapewi taji, asiposhindana kwa halali' (1 **Timotheo 2:5).*** Kuna kanuni za uzima katika Kristo, na moja yake ni kuwa unapaswa kuteseka kwa ajili ya Kristo.Uchukue msabala wako na uwe tayari kumfuata Kristo.

Wakati Paulo anapoandika kuhusu mkulima, haja yake ni kuwa mkulima anafanya kazi kwa bidii, wakati wa kupanda na wa kuvuna. Kisha, 'yampasa kuwa wa kwanza wa kupata fungu la matunda' **(6).** Paulo anamweleza Timotheo, 'fanya kwa bdii jinsi mkulima anavyofanya. Tia bidii wakati wa kupanda na wakati wa kuvuna.'

Paulo alikuwa mwaminifu kuhusu uwepo wa Kristo kwake, hata katika mateso yake. Hata wakati tunakuwa wanyonge bila imani, Mungu hubakia kuwa mwaminifu kwetu na hutusaidia, kwani hawezi kutuacha wale ambao tu sehemu yake. Ukweli wa Mungu husimama imara kama mwamba mkuu, na hakuna kitu kinachoweza kuutingisha. Ni jiwe la msingi ambalo maneno haya yameandikwa juu yake, *'Bwana awajua walio wake' **(19).***

Kumbuka hali ya mateso ya Paulo unaposoma maneno haya ya faraja kuu. Paulo anaandika kuwa inawezekana kuwa mgonjwa na dhaifu, kimawazo, akili na hata kiroho, kiasi kuwa hauna nguvu kuamini hata kuomba. Je unapotea katika hali hiyo? La hasha! Kifungu hiki kinasema kuwa hata kama sisi ni wanyonge katika maombi au tu wadhaifu kuamini, Mungu hatawahi kutuacha. Hata wakati hatuwezi kudumisha imani yetu, atakuwa kila mara mwaminifu kwetu.

Paulo anafunza kuhusu kusudi lake la maisha kwa mwaminifu kwa kutumia maelezo ya vyombo **(20-21).** Nyakati hizo, watu walikuwa na vyombo kubwa au birika,

nyumbani kwao. Baadhi ya vyombo hivyo vilitumika kwa kazi ya heshima, ilhali vingine vilitumika kwa kazi ambazo hazikuwa za heshima.

Paulo anasema kuwa, *'Timotheo, iko hivyo unapomfuata Kristo. Unaweza kuwa chombo ambacho kinatumika kwa kazi hazina heshima, au unaweza kugeuza tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani. Kisha utakuwa chombo ambacho ni cha kazi za heshima kilicho safi, kimfaacho Bwana.'*

Katika moja ya aya zinazofahamika sana katika waraka huu, Paulo anaandika kuwa, *'Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli'* ***(15).*** Paulo anasema, *'Timotheo, uwe na nidhamu na jitahidi ili kutokana na kujitolea kwako kujifunza, unathibitishwa na Mungu siku moja.'* Kila mara unafaa kuuliza, 'unajifunza, unajitahidi kujifunza neno la Mungu?

Hapo mwisho wa sura hii ya pili, Paulo anamshauri kijana Timotheo kuhusu jinsi ya kusadia watu kutatua shida zao. Leo, tunataja haki hiyo kama ushauri wa uchungaji. Katika nyakati za Timotheo na Paulo, kungekuwa na uchungaji. Nashangazwa na hali kuwa maneno yake ya mwisho, ambayo yalisema katika hali ya kutisha hivyo, wanamfuza Timotheo kuwa mchungaji mwema.

Paulo anamweleza Timotheo kuwa, shida ambazo zina watu anaowarekebisha ni kuwa wanaishi katika upinzani na mpango wa kipekee wa Mungu katika maisha yao. Wametegwa na Ibilisi **(26).** Kuna sababu nyingi kwa nini watu hufanya hivyo. Wanaweza kuwa wanajilinganisha na watu wengine, au kuwadhihaki wengine, au kujitolea kuongozwa na watu wengine. Hizi ni njia nyingi ambazo tunaweza kusema 'kijipotosha' kwa hali hiyo. Watu ambao wanapinga mpango wa Mungu juu yao watakuwa na shida nyingi na huzuni katika maisha yao.

Paulo anasema, *'Timotheo, ikiwa kwa upole, utulivu na uvumilivu utawasikiliza watu hao, tunda hizi za Roho zinafanya mlango kuwa wazi kwa Mungu kukusikia. Kisha utaweza kuwaamuru watu hao na kuweka mbele kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru'* ***(tazama Yohana 8:32).*** Haufai kamwe kukabiliana na watu hao, kwani jambo hilo linafunga mlango wako kwa Mungu na kuwaacha katika utumwa wa Shetani. Nafikiri kuwa hili ni moja na mambo mazuri sana kuwahi kuandikwa juu ya hoja hili la ushauri wa kiroho na uchungaji.

**Utafanya Nini Kuhusu Unachofahamu?**

Kina cha waraka huu kinapatikana katika **3:10-4:5.** Paulo anafahamu kuwa atauliwa, labda baada ya siku kadha au masaa kadha baada ya waraka huu kuandikwa nakupitishwa nje ya gereza. Anapoelezea juu ya Maandiko haya kwa Timotheo, tunapaswa kuhisi mvuto wa maneno yake. Haya ni maneno ya imani, mateso na shauku yake kwa Timotheo, na umuhimu wa kweli za Injili. Mara nyingi katika kifungu hiki, Paulo anasema kwa Timotheo, 'unajua…unajua…unajua….' Je, Timotheo anajuaje mambo hayo yote ambayo Paulo anamfahamisha kuwa anafahamu?
Jibu la wazi kwa swali hilo ni kuwa, Timotheo anajua mambo yote kwa sababu aliyatazamia katika maisha ya Paulo. Paulo anampa changa moto kwa swali hili: Je utafanyia nini yote unayojua?'

Paulo anatoa ushauri huu wa mwisho kwa Timotheo: *'kwa hivyo, nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na*

*usiokufaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti, nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza huduma yako. Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika'* ***(2Timotheo 4:1-5)***

Maneno haya ni changa moto kwetu wote kuwa waaminifu na wenye bidii kwa kazi ya Bwana, na kuamua vile utakavyofanyia kile unachofahamu. Uhusiano wa Paulo na Timotheo pia ni matumizi muhimu kwa wosia huu wa mwisho na agano la Paulo. Ikiwa bado u mchanga katika imani yako au huduma, basi unamwitaji Paulo. Na ikiwa umekomaa na labda u muumini shupavu au mchungaji, basi unakosa ikiwa hauwatambui baadhi ya waumini wachanga kama Timotheo.

**Maneno Ya Mwisho Ya Askari Mzee**

Maneno haya makuu ya changa moto yanafuatwa na mengine ambayo lazima yalivunja moyo wa Timotheo. Haya ndiyo maneno ya mwisho ya mmishionari mkuu, mchungaji, mwalimu, mwana thiolojia na mwandishi wa nusu ya sehemu ya agano jipya katika historia ya Kanisa:

*'Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake'* ***(2 Timotheo 6-8).***